BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2019

# MAARIFA YA JAMII

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI 2019

# MAARIFA YA JAMII

*Kimechapwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ........................................................................................................ iii

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI... 2

2.1. Sehemu A ........................................................................................... 2

2.1.1. Kipengele I: Uraia ........................................................................ 2
2.1.2. Kipengele II: Historia ..................................................................... 19
2.1.3. Kipengele III: Jiografia ................................................................... 35

2.2. Sehemu B ........................................................................................... 50

3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA ........................................................................................... 58

4.0 HITIMISHO ........................................................................................... 61

5.0 MAPENDEKEZO ................................................................................... 62

KIAMBATISHO ........................................................................................... 64

# DIBAJI

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2019 kwa somo la Maarifa ya Jamii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa watahiniwa, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu. Majibu ya watahiniwa katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha maarifa, stadi na mielekeo ambayo watahiniwa waliweza kupata au kutopata katika kipindi cha miaka saba ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, sababu mbalimbali zilizosababisha watahiniwa kuweza au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi zimeainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama za juu walikuwa na maarifa yaliyowawezesha kubaini matakwa ya maswali au kuhawilisha maarifa ilihali watahiniwa waliokuwa na uelewa mdogo hawakuweza kubaini matakwa ya maswali au kuhawilisha maarifa. Kimsingi, watahiniwa wengi waliopata alama za chini waliandika majibu yasiyo sahihi ilhali wengine hawakujibu baadhi ya maswali au walichagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo ya mtihani.

Uchambuzi wa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali walizoonesha watahiniwa wakati wa kujibu maswali zimeainishwa. Aidha, ulinganifu wa kiwango cha kufaulu kati ya mwaka 2018 na 2019 kwa kila mada umefanyika ili kuonesha kupanda au kushuka kwa kiwango cha kufaulu katika kila mada.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa dosari zilizoainishwa katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza ujuzi na maarifa kwa watahiniwa wanaotarajiwa kuhitimu elimu ya msingi miaka ijayo. Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



**Dkt. Charles E. Msonde**
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE 2019) ulifanyika tarehe 11 na 12 ya mwezi Septemba, 2019. Katika mtihani huo, somo la Maarifa ya Jamii lilifanyika tarehe 11/09/2019. Jumla ya watahiniwa **947,077** walisajiliwa kufanya mtihani huo ambapo watahiniwa **933,335** sawa na asilimia **98.6** walifanya mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii. Uchambuzi wa majibu ya mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa watahiniwa **714,341** sawa na asilimia **76.63%** walifaulu.

Somo la Maarifa ya Jamii katika mtihani wa PSLE 2019 lilikuwa na jumla ya maswali 40 ya kuchagua na 5 ya majibu mafupi yaliyokuwa yamegawanyika katika sehemu kuu mbili A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 40 ya kuchagua ambayo yalikuwa yamegawanyika katika vipengele vitatu. Kipengele cha I: Uraia – kilichokuwa na maswali 12, kipengele cha II: Historia – kilichokuwa na maswali 14 na kipengele cha III: Jiografia kilichokuwa na maswali 14. Sehemu B ilikuwa na maswali 5 ya majibu mafupi ambayo ni swali 1 la Uraia, maswali 2 ya Historia na maswali ya mwisho 2 ya somo la Jiografia.

Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu zote mbili. Aidha, katika swali la 1 - 40 watahiniwa walipewa machaguo matano katika kila swali, ambayo kati yake kulikuwa na jibu sahihi. Watahiniwa walitakiwa kuchagua jibu sahihi na kisha kuweka kivuli katika herufi ya jibu sahihi katika fomu maalum ya kujibia (OMR). Katika kujibu swali la 41 – 45 watahiniwa walielekezwa kuandika majibu yao katika nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi.

Katika taarifa hii, herufi ya jibu sahihi imewekewa alama ya nyota (*) katika majedwali na chati. Zaidi ya hayo, asilimia ya watahiniwa ambao hawakufuata maelekezo ya namna ya kujibu swali iliwekwa katika uchambuzi na kupewa jina "Mengine" ikimaanisha watahiniwa ambao hawakujibu kabisa swali husika au walichagua jibu zaidi ya moja kama inavyoonekana katika majedwali na chati.Katika uchambuzi huu, idadi ya watahiniwa na asilimia yao katika kila chaguo umeoneshwa. Ubora wa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika kila swali utategemea idadi ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi. Katika uchambuzi huu pia, sababu za watahiniwa kuchagua jibu, vipotoshi zimebainishwa.

Katika uchambuzi huu, ukokotoaji wa kiwango cha kufaulu utategemea idadi ya watahiniwa waliochagua au kuandika jibu sahihi kama ifuatavyo;

endapo watahiniwa asilimia 0 hadi 39 ndio watakaokuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali au mada hiyo utaelezwa kuwa ni hafifu. Kwa upande mwingine, endapo watahiniwa kati ya asilimia 40 hadi 59 watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali hilo utaelezwa kuwa ni wa wastani. Aidha, ufaulu katika swali au mada utaelezwa kuwa mzuri endapo watahiniwa asilimia 60 au zaidi watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI


### 2.1. Sehemu A

#### 2.1.1. Kipengele I: Uraia

**Swali la 1:** Kwa nini ni muhimu kuwa na wimbo wa shule?

A Ni utambulisho wa shule
B Huendeleza utamaduni wa taifa
C Huunganisha taifa
D Huhamasisha uzalendo
E Huwaenzi walimu

Swali hili lilitoka katika mada ya *Alama za Shule na za Taifa* na lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu umuhimu wa kuwa na wimbo wa shule. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 697,707 (74.75%) waliweza kuchagua jibu sahihi A, *Ni utambulisho wa shule.* Ni wazi kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu umuhimu wa wimbo wa shule kwani kila shule ina wimbo wake ambao mara nyingi huimbwa katika shule husika. Kwa misingi hiyo watahiniwa waliweza kuhamisha uzoefu wa maisha yao ya kila siku na kubaini jibu sahihi. Alama nyingine zinazotambulisha shule ni nembo ya shule, kauli mbiu ya shule na mipaka ya shule. Chati Na.1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1.




**Chati Na. 1** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 1.*


Chati Na. 1 inaonyesha kiwango kizuri cha kufaulu kwa watahiniwa kwani asilimia 74.75 walichagua jibu sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wengine walichagua majibu yasiyo sahihi kama ifuatavyo: watahiniwa 115,426 (12.37%) walichagua kipotoshi B *Huendeleza utamaduni wa taifa*; walichagua kipotoshi hiki walifikiri kuwa wimbo wa shule ni kielelezo cha utamaduni wa taifa. Vilevile,watahiniwa 33,781 (3.62%) walichagua kipotoshi C,*Huunganisha taifa.* Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya mchango wa wimbo wa shule na wa Taifa. Wimbo wa taifa unaweza kuunganisha taifa mfano ubeti wa "Mungu ibariki Tanzania"; na kwamba wimbo wa shule ni maalumu kwa ajili ya mazingira ya shule husika na sio kwa taifa zima. Watahiniwa 65,339 (7.00%) walichagua kipotoshi D *Huhamasisha uzalendo*; hawakuwa na ufahamu kuwa wimbo wa shule hutambulisha shule na hauhamasishi uzalendo. Uzalendo ni hali ya mtu kuipenda nchi yake na kuwa tayari kuilinda. Mwisho, watahiniwa 18,338 (1.96%) walichagua jibu lisilo sahihi E, *Huwaenzi walimu*. Watahiniwa hao wanaonesha kuwa walikuwa na uelewa mdogo kuhusu umuhimu wa wimbo wa shule na kwamba wimbo wa shule hauenzi walimu waliopo shuleni bali husaidia kuitofautisha shule moja na nyingine.

**Swali la 2:** Ipi ni kazi ya Afisa Mtendaji wa kijiji?

A Kuongoza vikao vyote vya serikali ya kijiji
B Kuteua wajumbe wa kamati mbalimbali
C Kusimamia uchaguzi wa serikali ya kijiji
D Kukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali katika kijiji
E Kutoa adhabu kwa wahalifu katika kijiji

Swali lilitungwa kutoka mada ya *Serikali za Mitaa* na liliwataka watahiniwa kubaini jukumu la Afisa Mtendaji wa kijiji. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa hafifu ambapo watahiniwa 107,120 (11.48%) waliweza kuchagua jibu sahihi C, *Kusimamia uchaguzi wa serikali ya kijiji*. Pamoja na kazi hiyo, Afisa Mtendaji wa Kijiji ana majukumu ya kusimamia mkutano mkuu wa kijiji kwa kushirikiana na mwenyekiti wa serikali ya kijiji, kusimamia upatikanaji wa huduma za kijamii katika eneo lake la utawala na kuongoza kamati mbalimbali za serikali ya kijiji. Chati Na.2 inaonesha kiwango hafifu cha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2.




**Chati Na. 2:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 2.*


Aidha, watahiniwa 403,924 (43.28%) waliochagua kipotoshi A, *Kuongoza vikao vyote vya kijiji;* hawakujua kuwa Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji ndiye huongoza mikutano ya serikali ya kijiji. Vilevile, watahiniwa 103,323 (11.07%) walichagua kipotoshi B, *Kuteua wajumbe wa kamati mbalimbali*. Watahiniwa hawakuelewa kuwa

Wajumbe wa kamati mbalimbali ya kijiji huteuliwa na halmashauri ya kijiji, na siyo Afisa Mtendaji wa kijiji. Watahiniwa 258,246 (27.67%) walichagua kipotoshi D, *Kukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali katika kijiji*. Vyanzo vya mapato ya kijiji husimamiwa na serikali ya kijiji na siyo Afisa Mtendaji wa Kijiji. Mwisho, watahiniwa 54,778 (5.87%) walivutiwa na kipotoshi E, *Kutoa adhabu kwa wahalifu katika kijiji.*Watahiniwa hawa hawakujua kuwa ulinzi na usalama katika kijiji husimamiwa na kamati ya ulinzi ya kijiji na wala siyo Afisa Mtendaji wa kijiji.

**Swali la 3**: Kipi ni kiashiria cha utawala bora katika jamii?

| | | | |
|---|---|---|---|
| A | Idadi kubwa ya wanasheria | B | Idadi kubwa ya magereza |
| C | Idadi kubwa ya wafungwa | D | Idadi ndogo ya wafungwa |
| E | Uongozi unaofuata sheria | | |

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Misingi ya Demokrasia* na lililenga kupima maarifa ya watahiniwa kuhusu viashiria vya utawala bora. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 785,918 (84.20%) walichagua jibu sahihi E,*Uongozi unaofuata sheria.* watahiniwa ambao walichagua jibu sahihi walikuwa na uelewa mzuri juu ya misingi ya utawala bora. Baadhi ya viashiria vingine vya utawala bora ni kuzingatia haki za binadamu, katiba ya kidemokrasia, ushirikishwaji wa wananchi, uhuru wa vyombo vya habari na uwazi. Chati Na.3 inaonesha kiwango kizuri cha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3.




**Chati Na. 3:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 3*


Chati Na. 3 inaonyesha kiwango kizuri cha ufaulu wa watahiniwa kwani asilimia 84.20 waliweza kuchagua jibu sahihi.

Chaguo A, *Idadi kubwa ya wanasheria,* lilivutia watahiniwa 53,946 (5.78%) ambao hawakujua kuwa, kuwa na idadi kubwa ya wanasheria hakuhakikishi uwepo wa utawala bora. Pia, watahiniwa 26,014 (2.79%) walichagua kipotoshi B, *Idadi kubwa ya magereza*, Watahiniwa 33,787 (3.62%) walichagua kipotoshi C, *Idadi kubwa ya wafungwa* na mwisho watahiniwa 28,604 (3.06%) walichagua kipotoshi D, *Idadi ndogo ya wafungwa*. Watahiniwa wote hawa walichagua vipotoshi kutokana na kutoelewa kuwa magereza ni sehemu ambayo watu waliopatikana na makosa hutunzwa, na uwepo wa idadi kubwa au ndogo ya wafungwa sio kiashiria cha utawala bora. Aidha, serikali duniani kote zina huduma za magereza bila kujali uwepo au kutokuwepo kwa utawala bora.

**Swali la 4:** Yupi kati ya wafuatao ni kiongozi wa sekretariati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

A Naibu spika
B Waziri Mkuu
C Katibu wa Bunge
D Spika
E Mwenyekiti wa Bunge

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye mada ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* na liliwataka watahiniwa kubaini kiongozi wa Sekretarieti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kilikuwa hafifu, ambapo watahiniwa 132,381 (14.18%) tu ndio walichagua jibu sahihi C, *Katibu wa Bunge*. Katibu wa Bunge ndiye mtendaji mkuu katika ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mshauri wa Spika katika mambo yote ya utawala na ndiye kiongozi wa Sekretarieti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jukumu la Sekretarieti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuhakikisha kuna ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Bunge. Chati Na.4 inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4.




**Chati Na.4:** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kiwango hafifu cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 4 kwani ni asilimia 14.18 tu walioweza kuchagua jibu sahihi.

Kwa upande mwingine, chaguo A, *Naibu Spika,* liliwavutia watahiniwa 165,292 (17.71%) ambao hawakuwa na ufahamu wa jukumu la Naibu Spika. Naibu spika huendesha vikao vya Bunge wakati Spika hayupo. Watahiniwa 323,487 (34.66%) walichagua kipotoshi B, *Waziri Mkuu* bila kujua kuwa Waziri Mkuu ni kiongozi mkuu wa shughuli zote za serikali Bungeni. Vilevile chaguo D, *Spika* lilivutia watahiniwa 243,511 (26.09%). Watahiniwa waliochagua jibu hili hawakuwa na uelewa kuwa Spika wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ndiye kiongozi mkuu wa shughuli zote za Bunge. Pia huwakilisha wabunge katika vikao vingine vyote nje ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwisho watahiniwa 62,300 (6.67%) ambao walichagua kipotoshi E *Mwenyekiti wa Bunge* hawakufahamu kuwa Mwenyekiti wa Bunge huongoza vikao vya Bunge endapo Spika na Naibu Spika hawapo. Kwa ujumla watahiniwa waliochagua vipotoshi hawakufahamu muundo wa uongozi wa sekretarieti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Swali la 5:** Ipi kati ya zifuatazo ni sifa za uchaguzi huru na wa haki?

A Kuwepo na waangalizi wa uchaguzi kutoka nchi nyingine
B Uhuru wa wapiga kura kushangilia barabarani
C Askari polisi kupewa mamlaka kuhesabu kura
D Watu kupiga kura kupitia sanduku la siri
E Watu kupiga kura kwa kunyosha mkono

**Jedwali Na. 1: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 154,036 | 87,772 | 96,702 | 484,852 | 103,133 | 6,848 |
| Asilimia ya watahiniwa | 16.50 | 9.40 | 10.36 | 51.95 | 11.05 | 0.73 |

Katika jedwali la 1 kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni cha wastani kwani asilimia 51.95 walichagua jibu sahihi.

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Demokrasia* na lilipima maarifa ya watahiniwa kuhusu sifa za uchaguzi huru na wa haki. Kama Jedwali Na. 1 linavyoonesha kufaulu katika swali hili kulikuwa kwa wastani ambapo watahiniwa 484,852 (51.95%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *watu kupiga kura kupitia sanduku la siri.* Sanduku la siri la kupigia kura ni mojawapo ya sifa za uchaguzi huru na wa haki. Sanduku la siri la kura humwezesha mpiga kura kutumia haki yake ya kidemokrasia kuchagua viongozi wake anaowapenda bila hofu au vitisho. Sifa nyingine za uchaguzi ulio huru na haki ni haki sawa kwa vyama vya siasa na wagombea, kampeni huru kwa vyama vyote vya siasa, kupewa nafasi sawa wakati wa kampeni ili kuwafikia wapiga kura nchi nzima, kuwepo kwa chombo huru cha kusimamia uchaguzi, uchaguzi usiobagua chama cha siasa au mgombea, kampeni huru kwa vyama vyote vya siasa na haki sawa kutumia vyombo vya habari ili kunadi sera za vyama wakati wa kampeni za uchaguzi.

Hata hivyo, watahiniwa wengine 154,036 (16.50%) walichagua kipotoshi A, *Kuwepo kwa waangalizi kutoka nje*. Watahiniwa hawakutambua kwamba waangalizi kutoka nje ya nchi hawahusiki katika usimamizi wa uchaguzi. Hivyo, uwepo wao hauhakikishi uwepo wa uchaguzi ulio huru na haki. Watahiniwa 103,133 (11.05%) walichagua jibu lisilo sahihi E, *Watu kupiga kura kwa kunyosha mkono,*

hawakujua kuwa, kunyosha mikono wakati wa kupiga kura hakutoi haki kwa watu kupiga kura kwa viongozi wanaowataka bila hofu au vitisho. Ukweli ni kwamba zoezi la kupiga kura kwa kunyosha mkono ni sehemu ya demokrasia ya moja kwa moja ambayo inafaa katika eneo dogo la kijiografia au idadi ndogo ya watu. Pia, watahiniwa 96,702 (10.36%) walichagua kipotoshi C, *Askali polisi kupewa mamlaka ya kuhesabu kura*. Katika uchaguzi huru na wa haki Jeshi la Polisi linawajibu wa kutoa ulinzi kwa wagombea wa vyama vyote vya siasa wakati wa mikutano ya kampeni za uchaguzi na siku ya kupiga kura.

Mwisho,watahiniwa 87,772 (9.40%) walichagua kipotoshi B, *Uhuru wa wapiga kura kushangilia barabarani.* Watahiniwa hao hawakutambua kuwa kushangilia barabarani/ mitaani siyo sifa ya uchaguzi huru na wa haki. Kitu cha muhimu ni taratibu za uchaguzi zinazozingatia maadili ya uchaguzi yaliyokubalika na wadau wote wa uchaguzi wakati wa uchaguzi.

**Swali la 6:** Ipi kati ya zifuatazo ni tahadhari ya kuchukua kabla ya kuvuka barabara sehemu ambayo hakuna alamamilia au taa za barabarani?

A Kuangalia kushoto na kulia kabla ya kuvuka barabara

B Kuangalia kulia, kushoto na kulia tena kabla ya kuvuka barabara


C Kuangalia nyuma, kulia, mbele na kushoto kabla ya kuvuka barabara

D Kuangalia mbele na nyuma kabla ya kuvuka barabara

E Kuangalia kulia, kushoto na kukimbia kuvuka barabara

Swali lilitungwa kutoka mada ya *Ulinzi na usalama katika ngazi ya Shule*/*Taifa*. Swali hili lililenga kupima uelewa wa watahiniwa juu ya tahadhari za usalama barabarani. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kilikuwa hafifu ambapo watahiniwa 357,640 (38.32%) tu ndio waliweza kuchagua jibu sahihi B, *kuangalia kulia, kushoto na kulia tena kabla ya kuvuka barabara.* Watahiniwa waliobaini jibu sahihi walikuwa na ufahamu wa tahadhari za usalama barabarani zinazoweza kuchukuliwa wakati wa kuvuka barabara upande wa pili. Tahadhari nyingine ni pamoja na waenda kwa miguu kutembea upande wa kulia wa

barabara. Katika maeneo ya mijini sehemu zenye barabara za lami waenda kwa miguu wanashauriwa kuvuka sehemu zenye alamamilia. Chati Na.5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6.




**Chati Na.5:** *Ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 6*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 326,017 (34.93%) walichagua jibu lisilo sahihi A, *Kuangalia kushoto na kulia kabla ya kuvuka barabara.* Pia watahiniwa 133,666 (14.32%) walichagua kipotoshi C, *Kuangalia nyuma, kulia, mbele na kushoto kabla ya kuvuka barabara.* Watahiniwa 61,239 (6.56%) walivutiwa na jibu lisilo sahihi E, *Kuangalia kulia, kushoto na kukimbia kuvuka barabara* na mwisho watahiniwa 50,098 (5.37%) walichagua kipotoshi D, *Kuangalia mbele na nyuma kabla ya kuvuka barabara.* Watahiniwa waliochagua vipotoshi A, C, D na E hawakuwa na ufahamu kuhusu tahadhari ya kuchukua wakati wa kuvuka barabarani. Watu wanapaswa kuwa waangalifu wanapopita barabarani Kwa miguu. Pia matumizi sahihi ya alama za onyo Kwa watumiaji wa barabara ili kuepusha ajali za barabarani ambazo husababisha ulemavu, uharibufu wa mali pamoja na vifo.

**Swali la 7:** Ipi kati ya zifuatazo ni sababu ya kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Kwanza ya Afrika Mashariki mwaka 1977?

A Nchi wanachama kuwa na makabila mengi
B Tofauti ya ukubwa wa nchi wanachama
C Tofauti za lugha
D Tofauti za kiitikadi kati ya nchi wanachama
E Tofauti za sarafu

**Jedwali Na. 2: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 116,834 | 106,193 | 176,795 | 453,376 | 72,524 | 7,621 |
| Asilimia ya watahiniwa | 12.52 | 11.38 | 18.94 | 48.58 | 7.77 | 0.82 |

Katika jedwali la 2 *kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni cha wastani kwani asilimia 48.58 walichagua jibu sahihi.*

Swali lilitungwa kutoka mada ya *Ushirikiano baina ya Tanzania na Mataifa Mengine* na lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu sababu ya kuvunjika kwa jumuiya ya kwanza ya Afrika Mashariki mwaka 1977. Kama Jedwali Na. 2 linavyoonesha ufaulu wa watahiniwa ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 453,376 (48.58%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *Tofauti za kiitikadi kati ya nchi wanachama*, watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tofauti za kiitikadi zilivyo sababisha kuvunjika kwa jumuiya hiyo. Tanzania ilikuwa inafuata itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea wakati Kenya na Uganda zilifuata itikadi za kibepari. Ikumbukwe kwamba dunia pia ilikuwa imegawanyika katika kambi mbili zilizokuwa zinapingana kiitikadi. Kambi ya kijamaa ikiongozwa na Urusi na kambi ya kibepari ikiongozwa na Marekani huku kila kambi ikijaribu kupanua wigo wa ushawishi wake duniani. Vita baridi kati ya kambi hizo mbili ilisababisha uhasama baina ya nchi na kutengeneza mazingira ya kutoaminiana yaliyokuwa na athari kubwa katika uhusiano wa kimataifa. Aidha, Uganda chini ya utawala wa dikteta Idd Amin ilikuwa na mgogoro wa mpaka na Tanzania baada ya Uganda kujaribu kutwaa sehemu ya ardhi ya Tanzania.

Kipotoshi C, *Tofauti za lugha* kiliwavutia watahiniwa 176,795 (18.94%). Watahiniwa hao hawakuwa na ufahamu wa lugha maarufu

zinazozungumzwa katika nchi wanachama wa Afrika ya Mashariki. Lugha ya Kiswahili inayozungumzwa na watu wengi katika nchi zote za Afrika ya Mashariki. Aidha, nchi zote wanachama ziliwahi kuwa makoloni ya waingereza hivyo lugha ya kiingereza ilizungumzwa pia na watu wengi katika eneo hili. Kutokana na hilo tofauti za lugha haikuwa hoja ya msingi ya kuvunjika kwa jumuiya ya Afrika Mashariki. Chaguo A, *Nchi wanachama kuwa na makabila mengi* liliwavutia watahiniwa 116,834 (12.52%). Watahiniwa hao hawakuwa na ufahamu kuwa uwepo wa makabila mengi hakikuwa chanzo cha kuvunjika jumuiya ya Afrika Mashariki. Chaguo B, *Tofauti ya ukubwa wa nchi wanachama* liliwavutia watahiniwa 106,193 (11.38%) ambao hawakujua kuwa tofauti ya ukubwa wa nchi miongoni mwa wanachama haikusababisha kuvunjika kwa jumuiya kwani makubaliano ya ushirikiano baina ya nchi wanachama yanajengwa kwa kuzingatia maslahi ya kila mwanachama.


Vilevile, watahiniwa 72,524 (7.77%) walichagua kipotoshi E, *Tofauti za sarafu* bila kujua kuwa nchi wanachama walitumia sarafu moja inayoitwa shilingi. Hivyo, haikuwa sababu ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Swali la 8:** Ni katika eneo lipi Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) limekuwa mstari wa mbele?

A Kujenga uchumi wa kijamaa katika nchi zinazoendelea
B Kupiga vita usafirishaji wa bidhaa kutoka nchi tajiri kwenda nchi maskini
C Kuimarisha mfumo wa chama kimoja katika nchi maskini
D Kusaidia wakimbizi katika nchi za Afrika
E Kueneza utandawazi duniani

Swali lilitungwa kutoka mada ya *Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni Nyingine* na lilipima maarifa ya watahiniwa kuhusu taasisi za kibenki za kimataifa ambazo ziko mstari wa mbele katika harakati za kueneza mfumo wa utandawazi. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kilikuwa hafifu kwani watahiniwa wachache tu 168,354 (18.04%) waliweza kubaini jibu sahihi E, *Kueneza utandawazi duniani.* Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu shughuli za taasisi kubwa za kibenki za kimataifa mfano Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Shirika la Fedha la Kimataifa limeshiriki kwa karibu sana katika juhudi za

kufufua uchumi wa nchi nyingi za Afrika kwa kutoa mikopo yenye masharti yanayolenga kuimarisha mfumo wa utandawazi katika nyanja zote za kisiasa na kiuchumi. Chati Na.6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8.





**Chati Na. 6:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 8.*

Kipotoshi A, *Kujenga uchumi wa kijamaa katika nchi zinazoendelea* kiliwavutia watahiniwa 392,133 (42.10%) kutokana na historia ya Tanzania ya kufuata itikadi ya Ujamaa. Hivyo, kuamini kuwa maslahi ya taasisi ya fedha ya kimataifa yanafanana na ya nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Kipotoshi B, *Kupiga vita usafirishaji wa bidhaa kutoka nchi tajiri kwenda nchi maskini,* kiliwavutia watahiniwa 109,076 (11.69%) ambao hawakuwa na ufahamu kuwa lengo la taasisi za fedha za kimataifa ni kulinda maslahi ya makampuni makubwa ya kimataifa ikiwa ni pamoja na soko la bidhaa kutoka nchi tajiri. Watahiniwa 102, 625 (11.00%) walichagua kipotoshi C, *Kuimarisha mfumo wa chama kimoja katika nchi maskini* hawakujua kuwa ushawishi wa mfumo wa chama kimoja ulipotea duniani baada ya kusambaratika kwa kambi ya mashariki iliyokuwa ikiongozwa na Urusi. Kwa upande mwingine, nchi za magharibi na taasisi zake za kimataifa zimekuwa zikiweka shinikizo kwa nchi zinazoendelea kuruhusu demokrasia ya vyama vingi.
Vilevile, chaguo D, *Kusaidia wakimbizi katika nchi za Afrika,* lilivutia watahiniwa 151,164 (16.20%) ambao hawakuwa na ufahamu kuwa kazi ya taasisi za kibenki za kimataifa au za ndani ni kutoa mikopo kwa masharti nafuu kwa nchi, taasisi au mtu binafsi. Jukumu la kusaidia wakimbizi liko mikononi mwa Shirika la Umoja wa Mataifa linalishughulikia wakimbizi UNHCR kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa na taasisi nyingine zisizo za kiserikali.

**Swali la 9:** Nyimbo, maigizo na mashairi vinawakilisha nini?

A Itikadi
B Matambiko
C Sanaa za ufundi
D Sanaa za maonyesho
E Jando na unyago

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utamaduni Wetu.* Lengo la swali lilikuwa ni kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu vielelezo mbalimbali vya utamaduni wetu. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 741,919 (79.49%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *Sanaa za maonyesho.* watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vielelezo vya utamaduni ambapo waliweza kutofautisha Sanaa za ufundi na Sanaa za maonesho. Hivyo, kutovutiwa na majibu mengine. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9.




**Chati Na.7** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 9.*


Chaguo A, *Itikadi,* liliwavutia watahiniwa 29,066 (3.11%) ambao hawakujua kuwa dhana ya itikadi ni msimamo wa kiuchumi, kisiasa ama kijamii unaokubaliwa na jamii fulani, hivyo, chaguo hilo halikuwa jibu sahihi. Kipotoshi B, *Matambiko* kilivutia watahiniwa 45,230 (4.85%) ambao pia hawakujua kuwa matambiko ni ibada inayofanywa na mtu kwa mizimu yake akiomba baraka. Kipotoshi C, *Sanaa za ufundi*, kiliwavutia watahiniwa 65,096 (6.97%) ambao walishindwa kutofautisha Sanaa za ufundi na Sanaa za maonesho. Hivyo, kuamini kuwa nyimbo, maigizo na mashairi vinawakilisha Sanaa za ufundi. Vilevile, kipotoshi

E, *Jando na unyago,* kilivutia watahiniwa wengi 47,405 (5.08%) ambao hawakubaini tofauti ya sanaa za maonesho na dhana ya jando na unyago. Jando na unyago ni mila ya kuwafunza vijana wa kike na kiume maadili na desturi ya jamii husika. Kwa ujumla, watahiniwa walioshindwa kuchagua jibu sahihi walikosa maarifa ya kutosha ya vielelezo mbalimbali vya utamaduni.

**Swali la 10:** Ni sekta ipi inatoa nafasi za ajira kwa watanzania walio wengi?

A Madini B Kilimo C Viwanda
D Biashara E Utalii

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Uchumi wetu* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini sekta inayotoa ajira kwa watanzania walio wengi. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 564,419 (60.47%) waliweza kuchagua jibu sahihi B, *Kilimo.* Idadi kubwa ya watahiniwa kubaini jibu sahihi inaonesha kuwa watahiniwa walio wengi wana maarifa ya kutosha kuhusu sekta inayotoa ajira kwa watanzania walio wengi. Ikumbukwe kwamba zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo kuendesha maisha yao. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10.





**Chati Na. 8:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 10.*

Chaguo A, *Madini,* lilivutia watahiniwa 40,967 (4.39%) kutokana na juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta hii na kulinda maslahi ya wachimbaji wadogo wa madini. watahiniwa walitumia uzoefu huo kuchagua kipotoshi hiki. Kipotoshi C, *Viwanda,* kimevutia watahiniwa 156,459 (16.76%) kutokana na juhudi za sasa za serikali za kujenga uchumi wa viwanda. Kipotoshi D, *Biashara,* kilivutia watahiniwa 128,265 (13.74%) kutokana na juhudi za serikali kuhamasisha ujasiriamali. Aidha, uwepo wa wafanyabiashara wadogowadogo katika sehemu za miji nchini umeshawishi baadhi ya watahiniwa kuamini kuwa biashara ni sekta inayotoa ajira kwa watanzania wengi. Vilevile, kipotoshi E, *Utalii,* kimevutia watahiniwa 38,353 (4.11%). Sekta ya utalii ni chanzo cha fedha nyingi za kigeni kwa taifa lakini haitoi ajira kwa kiwango sawa na sekta ya kilimo. Isitoshe, shughuli za utalii hufanyika katika maeneo machache tu yenye vivutio vya utalii wakati shughuli za kilimo hufanyika nchi nzima.

**Swali la 11:** Chombo kilichoanzishwa mwaka 1964 ili kulinda uhuru na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni

A Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.
B Jeshi la Magereza la Tanzania.
C Idara ya Uhamiaji Tanzania.
D Jeshi la Polisi la Tanzania.
E Jeshi la Mgambo la Tanzania.

Swali hili lilitungwa kutoka mada ya *Ulinzi na Usalama wa Taifa na rasilimali zake* na lilipima ufahamu wa watahiniwa kuhusu chombo kilichoanzishwa mwaka 1964 ili kulinda uhuru na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa 640,082 (68.58%) walichagua jibu sahihi A, *Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.* Watahiniwa walikuwa na ufahamu wa kutosha wa chombo kilichoanzishwa mwaka 1964 hivyo kutovutiwa na machaguo mengine yaliyokuwepo. Chati Na. 9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11.




**Chati Na.9:** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 11.*

Chaguo B*, Jeshi la Magereza la Tanzania,* liliwavutia watahiniwa 45,704 (4.90%) ambao hawakuwa na ufahamu kuwa jukumu la msingi la Jeshi la Magereza ni kulinda na kuwahifadhi wafungwa waliopatikana na makosa mbalimbali hivyo, halikuwa jibu sahihi. Kipotoshi C*, Idara ya Uhamiaji Tanzania,*kilivutia watahiniwa 69,463 (7.44%) ambao hawakuwa na ufahamu kwamba Idara ya uhamiaji ipo chini ya Wizara ya Mambo ya ndani yenye jukumu la kuratibu shughuli zote za uhamiaji nchini. Vilevile, kwa nafasi yake idara inashirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuhakikisha kuwa nchi ipo salama. Kipotoshi D, *Jeshi la Polisi la Tanzania,* kilivutia watahiniwa 129,344 (13.86%) ambao hawakujua kuwa jeshi la Polisi lipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani lenye majukumu ya kila siku ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Jukumu lingine ni kusimamia usalama barabarani. Vilevile, kipotoshi E, *Jeshi la Mgambo la Tanzania,* kilichaguliwa na watahiniwa 43,019 (4.61%) ambao hawakufahamu kuwa Jeshi la Mgambo hufanya kazi sawa na kazi za Polisi na lina ushirikiano wa karibu sana na Jeshi la Polisi.

Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua B, C, D, E walishindwa kutofautisha majukumu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na majukumu ya vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

Swali **la 12:** Nani anaongoza kikao cha Sekretarieti ya Mkoa?

A Katibu Tawala wa Mkoa
B Mkuu wa Mkoa
C Kamanda wa Polisi wa Mkoa
D Meya
E Mhasibu Mkuu wa Mkoa

**Jedwali Na. 3 Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 196,034 | 544, 272 | 41,437 | 104,706 | 39,059 | 5,835 |
| Asilimia ya watahiniwa | 21.00 | 58.31 | 4.44 | 11.43 | 4.18 | 0.63 |

Katika jedwali la 3 kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni cha wastani kwani asilimia 58.31 walichagua jibu sahihi.

Swali lilitungwa kutoka mada ya *Serikali Kuu* na lilipima maarifa ya watahiniwa kuhusu muundo wa uongozi wa serikali ya mkoa. Jedwali Na. 3 linaonesha kuwa kufaulu kwa watahiniwa kulikuwa wastani ambapo watahiniwa 544, 272 (58.31%) waliweza kuchagua jibu sahihi B, *Mkuu wa Mkoa.* Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuwa Mkuu wa Mkoa ni kiongozi wa Sekretariati ya Mkoa. Mkuu wa Mkoa huteuliwa na Rais na majukumu yake ni pamoja na kutekeleza kazi za Serikali Kuu ndani ya mkoa. Kazi ya Sekretarieti ya Mkoa ni kumsaidia Mkuu wa Mkoa kutekeleza majukumu yake ya kila siku katika mkoa.

Chaguo A, *Katibu Tawala wa Mkoa,* lilivutia watahiniwa 196,034 (21.00%) ambao hawakujua kuwa Katibu Tawala wa mkoa ni katibu wa vikao vya sekretarieti ya mkoa na ndiye msimamizi wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika mkoa. Kipotoshi C, *Kamanda wa Polisi wa Mkoa,*kilivutia watahiniwa 41,437 (4.44%) ambao hawakuwa na ufahamu kuwa jukumu la Kamanda wa Polisi wa mkoa ni kusimamia maswala ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao katika mkoa. Watahiniwa 106,706 (11.43%) walivutiwa na Kipotoshi D, *Meya.* Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha muundo wa serikali kuu na muundo wa serikali za mitaa. Nafasi ya meya ipo katika muundo wa serikali za mitaa. Vilevile kipotoshi E, *Mhasibu Mkuu wa Mkoa,*kilivutia watahiniwa 39,059 (4.18%). Chaguo hili halikuwa sahihi kwani mhasibu mkuu wa mkoa ana jukumu la kudhibiti matumizi ya fedha katika serikali ya mkoa.

### 2.1.2. Kipengele II: Historia

**Swali la 13:** Mataifa ya Ulaya yaliyokuwa yameshapitia mageuzi ya viwanda hadi mwishoni mwa karne ya 19 ni pamoja na

A Ufaransa, Italia na Ujerumani.
B Uingereza, Ujerumani na Marekani
C Marekani, Ujerumani na Ufaransa
D Marekani, Japani na Uingereza.
E Uingereza, China na Ufaransa

**Jedwali Na. 4: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 251,375 | 314,927 | 153,584 | 84,958 | 118,997 | 9,502 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 26.93 | 33.74 | 16.46 | 9.10 | 12.75 | 1.02 |

Katika jedwali la 4 kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni hafifu kwani ni asilimia 26.9 tu ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.

Swali liliwataka watahiniwa kubaini kundi linalounda mataifa ya kibepari ya Ulaya yaliyokuwa yameshapitia mageuzi ya viwanda hadi mwishoni mwa karne ya 19. Ufaulu katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani watahiniwa 251,375 (26.93%) tu waliweza kuchagua jibu sahihi A, *Ufaransa, Italia na Ujerumani*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mataifa ya kibepari ya Ulaya yaliyokuwa yameshapitia mageuzi ya viwanda hadi mwishoni mwa karne ya 19.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 672,466 (72.05%) walichagua vipotoshi: B, *Uingereza*; *Ujerumani na Marekani*; C, *Marekani; Ujerumani na Ufaransa;* D, *Marekani, Japani na Uingereza* na E, *Uingereza, China na Ufaranza.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kwamba watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mataifa ya Ulaya yaliyokuwa yameshapitia mageuzi ya viwanda hadi mwishoni mwa karne ya 19. Kwa ujumla, watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa “Japani”, “China” na “Marekani” sio mataifa ya Ulaya.

**Swali la 14:** Familia ya  Ndugu Kamchape inajumuisha watoto wake, mkewe na binamu yake. Hii ni familia ya aina gani?

A  Familia ya wake wengi
B  Familia ya baba, mama na watoto
C  Familia ya baba, mama, watoto na ndugu wengine
D  Familia ya mzazi mmoja
E  Familia ya watoto peke yao

**Jedwali Na. 5: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahinwa | 29,143 | 76,544 | 753,329 | 49,205 | 21,539 | 3,583 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 3.12 | 8.20 | 80.71 | 5.27 | 2.31 | 0.38 |

Katika jedwali la 5 kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni kizuri kwani asilimia 80.7 walichagua jibu sahihi.

Swali lilitungwa kutoka mada ya *Familia Yetu*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini aina ya familia ya ndugu Kamchape inayojumuisha watoto wake, mkewe na binamu yake. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni mzuri kwani watahiniwa 753,329 (80.71%) waliweza kuchagua jibu sahihi A, *Familia ya baba, mama watoto na ndugu wengine*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za familia.


Kwa upande mwingine, watahiniwa 176,431 (18.90%) walichagua machaguo yasiyo sahihi jambo linaloashiria kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu familia na vipengele vyake. Watahiniwa hao walipashwa kuelewa kuwa aina hii ya familia (pana) ni familia ya baba, mama, watoto na ndugu wengine. Aina hii ya familia pana imeenea sana katika bara la Afrika. Ndugu huhusisha babu, bibi, mjomba, shangazi, binamu, mpwa, shemeji, mjukuu na kitukuu.

**Swali la 15 :** Mtoto wa mjomba huitwa

A  mpwa.  B  mjukuu.  C  shangazi.
D  binamu.  E  dada.

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye mada ya *Familia Yetu* na liliwataka watahiniwa kubaini jina sahihi kwa mtoto wa mjomba. Kwa ujumla,

kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 758,090 (81.22%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *binamu.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mahusiano ya familia. Chati Na. 11: Inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 10** *kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 15*

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 172,040 (18.43%) waliochagua vipotoshi: A, *mpwa,* B, *mjukuu*; C, *shangazi* na E, *dada.* Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mahusiano katika familia. Watahiniwa hao walipashwa kuelewa kuwa *mpwa* ni mtoto wa kaka au dada yako; *mjukuu* ni mtoto wa mtoto wako ; *shangazi* ni dada wa baba yako na *dada* ni msichana au mwanamke mnayechangia baba.

**Swali la 16 :** Ni nani huhakikisha kuwa shughuli za kila siku shuleni zinatekelezwa ipasavyo?

| | | | |
|---|---|---|---|
| A | Mwalimu wa nidhamu | B | Kiranja mkuu |
| C | Mwalimu wa somo | D | Mwalimu mkuu |
| E | Kiranja wa zamu | | |

**Jedwali Na. 6: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 98,092 | 153,655 | 31,366 | 574,760 | 71,420 | 4,050 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 10.51 | 16.46 | 3.36 | 61.58 | 7.6.5 | 0.43 |

Katika jedwali la 6 kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni hafifu kwani ni asilimia 10.51 tu ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.

Swali lilitoka katika mada ya *Shule Yetu.* Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini mtu anayehakikisha kuwa shughuli za kila siku shuleni zinatekelezwa ipasavyo. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 574,760 (61.58%) walichagua jibu sahihi D, *mwalimu mkuu.* Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa kuwa majukumu ya mwalimu mkuu ni pamoja na kuhakikisha kuwa shughuli za kila siku shuleni zinatekelezwa ipasavyo, walimu wote wana tekeleza majukumu yao na wanafanya kazi katika mazingira bora.

Pamoja na hayo, jumla ya watahiniwa 339,628 (37.99%) walichagua vipotoshi A, *Mwalimu wa nidhamu;* kipotoshi B, *Kiranja mkuu;* kipotoshi C, *Mwalimu wa somo* na E, *Kiranja wa zamu*. Uchaguzi wa machaguo yasiyo sahihi umetokana na watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu majukumu na wajibu ya viongozi mbalimbali katika ngazi ya shule.


**Swali la 17:** Mfano wa kupinga kwa njia ya vita uvamizi wa kikoloni ulikuwa ni

A vita vya Maji maji dhidi ya Waingereza katika Tanganyika.
B vita vya Washona na Wandebele dhidi ya Wajerumani.
C vita vya Wanama na Waherero dhidi ya Waingereza.
D vita vya Waasante dhidi ya Wajerumani.
E vita vya Wamandika dhidi ya Wafaransa.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uvamizi wa Kikoloni*. Swali liliwataka watahiniwa kubaini mfano wa kupinga kwa njia ya vita uvamizi wa kikoloni. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa kiwango dhaifu kwa sababu watahiniwa 878,190 (94.09%) walichagua vipotoshi A, B, C na D.

Kipotoshi A, *vita vya Maji maji dhidi ya Waingereza katika Tanganyika* kiliwavutia watahiniwa 452,385 (48.47%). Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kupinga kwa njia ya vita uvamizi wa kikoloni (vita vya maji maji) kulikofanywa na jamii wa Wangindo, Wamatumbi, Wapogoro na Wazaramo kusini mwa Tanganyika lakini hawakujua taifa la Ulaya lililohusika na kipindi ambacho vita hiyo ilitokea. Kwa ufupi, watahiniwa hawa walitarajiwa kuelewa kuwa vita vya Maji maji vilipiganwa dhidi ya Wajerumani kuanzia mwaka 1905 hadi 1907 na siyo dhidi ya Waingereza waliotawala Tanganyika kuanzia mwaka 1920 baada ya Ujerumani kushindwa katika Vita vya Kwanza vya Dunia.

Kipotoshi kingine kilichowavutia zaidi ya robo (28.77%) ya watahiniwa ni B, *vita vya Washona na Wandebele dhidi ya Wajerumani.* Chaguo hilo halikuwa sahihi kwa sababu jamii ya Washona na Wandebele walipigana dhidi ya Waingereza kwenye vita vilivyojulikana kama "vita vya Chimurenga" katika Rhodesia ya Kusini (Zimbabwe) na siyo dhidi ya Wajerumani. Zimbabwe ilikuwa koloni la Waingereza hivyo isingewezekana kwa Washona na Wandembele kupigana dhidi ya Wajerumani ambao hawakugombania Zimbabwe. Chati Na.11 inaonesha kufaulu wa watahiniwa katika swali la 17.




**Chati Na. 11** *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 17.*

Kipotoshi C, *vita vya Wanama na Waherero dhidi ya Waingereza* kilivutia watahiniwa 111,729 (11.97%). Hili halikuwa jibu sahihi kwa sababu jamii ya Wanama na Waherero nchini Namibia walipigana dhidi ya Wajerumani na siyo dhidi ya Waingereza.

Jumla ya watahiniwa 45,522 (4.88%) walichagua kipotoshi D, *vita vya Waasante dhidi ya Wajerumani*. Hilo halikuwa jibu sahihi kwa sababu Waasante hawakupigana vita dhidi ya Wajerumani bali walipigana vita dhidi ya Waingereza. Kwa ujumla, tunachojifunza kutokana na machaguo haya ni kwamba watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu jamii za Afrika zilizopigana vita dhidi ya dola za Ulaya katika kipindi cha kugombania na kugawana bara la Afrika.

Hata hivyo, watahiniwa 46,457 (4.98%) waliweza kuchagua jibu sahihi E, *vita vya Wamandika dhidi ya Wafaransa.* Chaguo hili linaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu jamii mbalimbali za Afrika zilizopigana dhidi ya uvamizi wa kikoloni uliofanywa na mataifa ya kibepari ya Ulaya.

**Swali la 18:** Katibu wa Halmashauri ya kijiji anajulikana kama

A Mwalimu mkuu.
B Mwenyekiti wa kijiji.
C Mtendaji wa kijiji.
D Mwenyekiti wa halmashauri ya kijiji.
E Mwenyekiti wa mtaa.

**Jedwali Na. 7: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 36,754 | 173,682 | 381,181 | 291,396 | 44,988 | 5,342 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 3.94 | 18.61 | 40.84 | 31.22 | 4.82 | 0.57 |

Katika jedwali la 7 kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni cha wastani kwani asilimia 40.8 walichagua jibu sahihi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Kijiji Chetu.* Swali liliwataka watahiniwa kubaini mtu mwenye cheo cha Katibu wa Halmashauri ya kijiji. Kiwango cha ufaulu kwa ujumla kilikuwa wastani kwani watahiniwa 381,181 (40.84%) waliweza kuchagua jibu sahihi C, *Mtendaji wa kijiji*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu uongozi katika ngazi ya kijiji. Kati ya vipotoshi vyote, kipotoshi D, *Mwenyekiti wa halmashauri ya kijiji* ,kiliwavutia watahiniwa wengi (219,396 sawa na asilimia 31.22). Kipotoshi hiki huenda kiliwavutia watahiniwa hao kwa sababu ya kuhusianisha maneno *halmashauri ya kijiji* ambayo yametumika kwenye mzizi wa swali na kwenye chaguo D.

Kipotoshi B, *Mwenyekiti wa kijiji* kiliwavutia watahiniwa 173,682 (18.61%). Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya majukumu ya Mtendaji wa kijiji na yale ya Mwenyekiti wa kijiji.

Kipotoshi A, *Mwalimu mkuu,* na E, *Mwenyekiti wa mtaa* vilichaguliwa na watahiniwa wenye uelewa mdogo juu ya uongozi katika ngazi ya kijiji. Kwa ujumla, inaweza kuhitimishwa kuwa zaidi ya nusu (58.59%) ya watahiniwa hawakuwa na uelewa kuhusu mada ya *Kijiji Chetu*.

**Swali la 19:** Mojawapo ya changamoto iliyoyakumba mataifa ya Ulaya baada ya mageuzi ya viwanda ilikuwa.


A Kuzorota kwa viwanda kutokana na Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia katika karne ya 19.
B Mahitaji makubwa ya mitaji kutoka katika makoloni.
C Mahitaji ya masoko kwa ajili ya bidhaa zao za viwandani.
D Kukua kwa biashara ya utumwa katika karne ya 20.
E Mahitaji ya teknolojia kwa ajili ya upanuzi wa viwanda vyao.

Swali lilitoka katika mada ya *Uvamizi wa kikoloni Afrika tangu mwaka 1880.* Swali liliwataka watahiniwa kubaini mojawapo ya changamoto zilizoyakumba mataifa ya Ulaya baada ya mageuzi ya viwanda. Ufaulu katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani ni watahiniwa 350,522 (37.56%) tu waliweza kuchagua jibu sahihi C, *Mahitaji ya masoko kwa ajili ya bidhaa zao za viwandani.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mahitaji yaliyotokana na kukua kwa viwanda.

Hata hivyo, watahiniwa 320,956 (34.39%) walichagua kipotoshi A, *kuzorota kwa viwanda kutokana na Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia katika Karne ya 19*. Watahiniwa hawa walipashwa kuelewa kuwa mapinduzi ya viwanda yalitokea katika karne ya 19 na Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia ilitokea katika Karne ya 20, hivyo isingewezekana kwa tukio lililotokea karne ya 20 kuleta changamoto kwa mataifa ya Ulaya kwenye karne ya 19. Majibu yaliyotolewa na watahiniwa hawa yanaonesha kuwa walishindwa kuhusianisha matukio ya kihistoria na vipindi vyake.

Vile vile, watahiniwa 100,879 (10.81%) walichagua kipotoshi E, *Mahitaji ya teknolojia kwa ajili ya upanuzi wa viwanda vyao*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki ulisababishwa na uelewa mdogo wa watahiniwa kuhusu *mahitaji ya viwanda*. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kwamba mahitaji ya teknolojia kwa ajili ya upanuzi wa viwanda vya Ulaya haikuwa changamoto kwa mapinduzi ya viwanda kwa mataifa ya Ulaya.

Kipotoshi B, *Mahitaji makubwa ya mitaji kutoka katika makoloni* kilichaguliwa na watahiniwa 68,061 (9.01%) na wengine 68,342 (7.32%) walichagua kipotoshi D *Kukua kwa biashara ya utumwa katika Karne ya 20*. Watahiniwa hawa walipashwa kuelewa kuwa mahitaji makubwa ya mitaji kutoka katika makoloni haikuwa changamoto kwa mataifa ya Ulaya kwa kuwa walikuwa na mitaji ya ziada kwa ajili ya kuwekeza katika makoloni yao ili waweze kupata faida zaidi. Kipotoshi D, *Kukua kwa biashara ya utumwa katika Karne ya 20* kilichaguliwa na watahiniwa ambao hawakuwa na maarifa kuhusu kukomeshwa kwa biashara ya watumwa. Mapinduzi ya viwanda Ulaya ndicho kilikuwa kiini cha kukomeshwa kwa biashara ya watumwa katika karne ya 19. Hivyo, siyo sahihi kuhusisha madhara ya mapinduzi ya viwanda Ulaya na kukua kwa biashara ya watumwa katika karne ya 20. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 19 umeoneshwa katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12**: *Kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 19*

**Swali la 20:** Ni katika makoloni yapi ya Ujerumani ambayo mfumo wa utawala wa moja kwa moja ulitumika?

A Tanganyika, Naijeria na Kameruni
B Tanganyika, Zimbabwe na Uganda
C Tanganyika, Zimbabwe na Misri
D Tanganyika, Togo na Kameruni
E Tanganyika, Naijeria na Ghana

**Jedwali Na. 8: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 125,165 | 309,838 | 116,796 | 159,798 | 213,036 | 8,710 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 13.41 | 33.20 | 12.51 | 17.12 | 22.83 | 0.93 |

Katika jedwali la 8 kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni hafifu kwani ni asilimia 17.1 tu walichagua jibu sahihi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utawala wa Kikolon Afrika*. Swali liliwataka watahiniwa kubaini makoloni ya Ujerumani ambayo mfumo wa utawala wa moja kwa moja ulitumika. Ufaulu wa swali hili ulikuwa dhaifu kwani watahiniwa 764,835 (81.95%) hawakuweza kuchagua jibu sahihi. Jumla ya watahiniwa 309,838 (33.20%) walichagua kipotoshi B, *Tanganyika, Zimbabwe na Uganda.* Chaguo hili halikuwa sahihi kwa kuwa *Zimbabwe na Uganda* zilikuwa makoloni ya Uingereza hivyo ilikuwa ni vigumu kwa utawala wa moja kwa moja wa Wajerumani kutumika katika koloni ambalo halikuwa chini ya Wajerumani.

Jumla ya watahiniwa 213,036 (22.83%) walivutiwa na kipotoshi E, *Tanganyika, Naijeria na Ghana*. Naijeria na Ghana yalikuwa makoloni ya Uingereza ambayo mfumo wa utawala usiokuwa wa moja kwa moja ulitumika. Kipotoshi A, Tanganyika, Naijeria na Kameruni na C, Tanganyika, Zimbabwe na Misri zilichaguliwa na asilimia 13.41 na asilimia 12.51 ya watahiniwa mtawalia. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa Naijeria, Zimbabwe na Misri hayakuwa makoloni ya Wajerumani. Hivyo, isingewezekana kwa mfumo wa utawala wa Wajerumani wa moja kwa moja kutumika kwenye makoloni ya Waingereza.

Zaidi ya hapo, jumla ya watahiniwa 159,798 (17.12%) walichagua jibu sahihi D, *Tanganyika, Togo na Kameruni*. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mgawanyo wa bara la Afrika miongoni mwa mataifa ya Ulaya.

**Swali la 21.** Ni kipi kilisababisha uchumi wa kikoloni katika Afrika?

A Biashara ya utumwa
B Mageuzi ya viwanda
C Azimio la Arusha
D Vita vya Kwanza vya Dunia
E Ukoloni mamboleo

**Jedwali 9: Idadi na wastani wa watahiniwa katika kila chaguo**

| Machaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 345,460 | 274,200 | 111,725 | 101,593 | 93,715 | 6,650 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 37.01 | 29.38 | 11.97 | 10.88 | 10.04 | 0.71 |

Swali lilitoka katika mada ya Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu liliwataka watahiniwa kubaini kilichosababisha uchumi wa kikoloni katika Afrika. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa dhaifu kwani watahiniwa (69.91%) walichagua vipotoshi A, *Biashara ya utumwa,* C, *Azimio la Arusha, D, Vita vya Kwanza vya Dunia* na E, *Ukoloni mamboleo.*

Jumla ya watahiniwa 345,460 (37.01%) walivutiwa na kipotoshi A, *Biashara ya utumwa*. Kipotoshi ‘Biashara ya utumwa’ kilichaguliwa na wanafunzi walioshindwa kuelewa mchango wa mapinduzi ya viwanda katika kutawaliwa kwa Bara la Afrika. Afrika ilitawaliwa na mataifa ya ulaya ili kupata masoko na malighafi kwa ajili ya viwanda vyao. Vipotoshi C, *Azimio la Arusha, D, Vita vya Kwanza vya Dunia E, Ukoloni mamboleo* viliwavutia watahiniwa asilimia 11.97, 10.88 na 10.04 mtawalia. Watahiniwa hao walipashwa kuelewa kuwa Azimio la Arusha na Ukoloni mamboleo ulikuja baada ya uhuru- kipindi ambapo uchumi wa kikoloni ulishaondolewa katika nchi nyingi za Afrika.

**Swali la 22:** Mahindi, mihogo na korosho zililetwa Tanganyika na nani?

A Waingereza
B Wadachi
C Waarabu
D Wajerumani
E Wareno

Swali hili lilitoka katika mada ya uhusiano wa Jamii za kitanzania na Jamii nyingine za Kiasia na kizungu, liliwataka watahiniwa kubaini watu walioleta mahindi, mihogo na korosho Tanganyika. Jibu sahihi ni E, *Wareno* lakini watahiniwa wengi (627,611) sawa na asilimia (67.28%) walishindwa kutoa jibu sahihi kwa kuwa walichagua vipotoshi A, B, C na D.

Kipotoshi C, *Waarabu* kiliwavutia watahiniwa 195,147 (20.91%) walioshindwa kutofautisha kati ya mazao yaliyoletwa na Waasia na yale yaliyoletwa na Wazungu. Watahiniwa hawa walipashwa kuelewa kuwa Waarabu hawakuleta mahindi, mihogo au korosho Tanganyika, bali walileta nazi, mpunga na ngano.

Vile vile, jumla ya watahiniwa 157,616 (16.89%) walichagua kipotoshi D, Wajerumani. Watahiniwa hao hawakuwa sahihi kwa sababu Wajerumani hawakuleta mahindi, miogo na korosho bali walileta katani. Vile vile, kipotoshi A, *Waingereza* na D, *Wajerumani* kila kimoja kilivutia watahiniwa asilimia 16.89. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kwamba sio Waingereza wala Wajerumani walileta mahindi, mihogo na korosho Tanganyika. Zao pekee ambalo Wajerumani wanaweza kusifiwa kulileta inchini Tanganyika ni katani.

Jumla ya watahiniwa 108,199 (11.59%) walichagua B, *Wadachi.* Chaguo hili lilichaguliwa na watahiniwa wenye uelewa mdogo kuhusu watu na aina ya mazao waliyoleta Tanganyika. Kwa ufupi, uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu muingiliano kati ya jamii ya Waafrika, Waasia na Wazungu na madhara yaliyotokana na mwingiliano huo.

Pamoja na hayo, watahiniwa 305,732 (32.76%) waliweza kuchagua jibu sahihi E, Wareno. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mazao yaliyoletwa Tanganyika na Waasia na Wazungu kutokana na muingiliano wao na Waafrika.

**Swali la 23:** Lipi ni jina la mwanasayansi aliyeelezea kuhusu mabadiliko ya umbile la binadamu ?


A Vasco Da Gama
B Charles Darwin
C Louis Leakey
D David Livingstone
E Bartholomew Diaz

Swali lilitoka katika mada ya *Asili na Chimbuko la Binadamu* Swali liliwataka watahiniwa kutaja jina la mwanasayansi aliyeelezea kuhusu mabadiliko ya umbile la binadamu. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wastani kwani watahiniwa 457,226 (48.99%) waliweza kuchagua jibu sahihi B, *Charles Darwin*. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wakutosha kuhusu mnadharia maarufu aliyefanya utafiti kuhusu chimbuko la binadamu.

Zaidi ya robo ya watahiniwa (27.35%) walichagua kipotoshi C, Louis Leakey. Uchaguzi wa kipotoshi hiki kwa asilimia hii ndogo ya watahiniwa kunaonesha kwamba watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya Charles Darwin (mwanasayansi asilia) na Louis Leakey (mtaalamu wa mambo ya kale). Watahiniwa hao walipashwa kuelewa kuwa Louis Leakey hakuelezea chimbuko la binadamu bali alivumbua fuvu la Zinjanthropus katika Bonde la Olduvai mwaka 1959.

Kipotoshi A, *Vasco Da Gama,* E, *Bartholomew Diaz* viliwavutia watahiniwa 69,691 (7.47%) na 55,797 (5.98%) mtawalia. Machaguo hayo hayakuwa sahihi kwa sababu Vasco Da Gama na Bartholomew Diaz walikuwa ni mabaharia wa Kireno waliotumwa na Mfalme Henry (the Navigator) kutafuta njia ya kwenda India (Asia). Hivyo, kinachojidhihirisha kutokana na machaguo haya yasiyo sahihi ni kwamba watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu muingiliano kati ya jamii ya Waafrika, Waasia na Wazungu na pia chimbuko na mabadiliko ya binadamu.

Watahiniwa wengine 89,785 (9.62%) walichagua kipotoshi D, *David Livingstone*. David Livingstone alikuwa mpelelezi na mmisionari maarufu Afrika ya Mashariki katika karne ya 19. Hivyo, watahiniwa waliochagua chaguo hilo walikosa maarifa kuhusu mtu maarufu na bingwa aliyeelezea chimbuko la binadamu au yule ambaye kazi yake ilipelekea kutawaliwa kwa Afrika Mashariki na Wazungu katika karne ya 19. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 13




**Chati Na. 13**: *Kufaulu wa watahiniwa katika swali la 23.*

**Swali la 24 :** Lipi kati ya matukio yafuatayo lilitokea Ulaya kati ya karne ya 18 na 19 ?

A Kuanzishwa kwa Jumuia ya Mataifa
B Kuzuka kwa vita kuu ya Kwanza ya Dunia
C Kuwasili kwa mabaharia wa kireno katika rasi ya Tumaini Jema
D Kukua kwa mapinduzi ya viwanda
E Kunzishwa kwa Benki ya Dunia

Swali liliwataka watahiniwa kubaini tukio lilitokea Ulaya kati ya karne ya 18 na 19. Ufaulu katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani asilimia 65.84 ya watahiniwa walishindwa kuchagua jibu sahihi.

Robo ya watahiniwa (sawa na asilimia 25.03%) walivutiwa na kipotoshi B, *Kuzuka kwa vita kuu ya Kwanza ya Dunia*. Hili halikuwa jibu sahihi kwa sababu vita kuu ya Kwanza ya Dunia haikutokea kati ya karne ya 18 na 19 bali ilitokea karne ya 20 (kuanzia 1914 hadi 1918).

Kipotoshi C, Kuwasili kwa mabaharia wa Kireno katika rasi ya Tumaini Jema kilichaguliwa na watahiniwa 188,723 sawa na asilimia 20.22. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kwamba mabaharia wa Kireno waliwasili katika rasi ya Tumaini Jema katika karne ya 15 na siyo kati ya karne ya 18 na 19

Jumla ya watahiniwa 134,201 (14.38%) walichagua kipotoshi A, Kuanzishwa kwa Jumuia ya Mataifa. Hilo halikuwa chaguo sahihi kwani

Jumuia ya Mataifa ulianzishwa mwaka 1920 (karne ya 20) na sio kati ya karne ya 18 na 19. Watahiniwa wachache 58,053 (6.22%) walichagua kipotoshi E, Kuanzishwa kwa Benki ya Dunia. Uchaguzi wa kipotoshi hicho kinaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu matukio ya kihistoria na athari zake kati ya karne 18 na 20. Benki ya Dunia ilianzishwa baada ya vita kuu ya Pili ya Dunia mwaka 1945.

Hata hivyo, watahiniwa 311,436 (33.37%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *Kukua kwa mapinduzi ya viwanda.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matukio ya kihistoria na vipindi yalipotokea.

**Swali la 25:** Ni Taasisi zipi za Umoja wa Mataifa zilishinikiza nchi za Kiafrika kufuata mfumo wa vyama vingi?

A Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia
B Mkutano Mkuu na Mahakama ya Haki ya Kimataifa
C Shirika la Fedha la Kimataifa na Baraza la Usalama
D Sekretarieti na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa
E Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa na Mkutano Mkuu

Swali lilitoka katika mada ya *Ushirikiano wa Kimataifa*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini taasisi za Umoja wa Mataifa zilishinikiza nchi za Kiafrika kufuata mfumo wa vyama vingi. Swali hili lilikuwa na ufaulu dhaifu kwani watahiniwa asilimia 75.30 hawakuweza kuchagua jibu sahihi.

Kipotoshi E, *Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa na Mkutano Mkuu* kilivutia asilimia 243,144 (26.05%). Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha kati ya mashirika na taasisi za Umoja wa Mataifa. Kwa ujumla, yote hayo hayakuwa na mchango wowote katika kushinikiza nchi za Afrika kufuata mfumo wa vyama vingi.

Vilevile, jumla ya watahiniwa 216,676 (23.22%) walichagua kipotoshi D, Sekretariati na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa Sekretariati ni shirika na siyo taasisi ya Umoja wa Mataifa. Sekretariati inaundwa na watumishi wa umma wa Mataifa chini ya uongozi wa Katibu Mkuu. Kwa ujumla,

Sekretariati na Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO) ni taasisi ambayo haikuzishinikiza nchi za Kiafrika kufuata mfumo wa vyama vingi.

Jumla ya watahiniwa 127,081 (13.62%) walichagua kipotoshi B, Mkutano Mkuu na Mahakama ya Haki ya Kimataifa. Hilo halikuwa jibu sahihi kwa sababu mkutano mkuu na Mahakama ya Haki ya Kimataifa siyo taasisi bali ni vyombo vya Umoja wa Mataifa.

Kipotoshi C, Shirika la Fedha la Kimataifa na Baraza la Usalama kilivutia watahiniwa 115,945 (12.42%). Watahiniwa hao walishindwa kufahamu kwamba Baraza la Usalama siyo taasisi bali ni Shirika la Umoja wa Mataifa.

Pamoja na hayo, watahiniwa 219,847 (23.55%) walichagua jibu sahihi A, *Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia.* Watahiniwa hao walielewa jinsi Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB) zilivyotumia uanzishwaji wa mfumo wa vyama vingi kama kigezo cha kutoa mikopo na misaada kwa nchi zinazoendelea.

**Swali la 26:** Ni akina nani walikuwa waanzilishi wa Jumuia mpya ya Afrika Mashariki?

A Julius Nyerere, Jomo Kenyata na Milton Obote
B Julius Nyerere, Daniel Moi na Yoweri Museveni
C Jakaya Kikwete, Daniel Moi na Yoweri Museveni
D Benjamin Mkapa, Uhuru Kenyatta na Yoweri Museveni
E Yoweri Museveni, Daniel Moi na Benjamin Mkapa

Swali hili liliwataka watahiniwa kubaini majina ya viongozi waanzilishi wa Jumuia mpya ya Afrika Mashariki. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa dhaifu kwani watahiniwa 926,654 (84.75%) hawakuweza kuchagua jibu sahihi.


Kipotoshi A, Julius Nyerere, Jomo Kenyata na Milton Obote kiliwavutia zaidi ya nusu ya watahiniwa (487,309 sawa na asilimia 52.21) waliojibu swali hili. Watahiniwa hawa walivutiwa na kipotoshi hiki kwa sababu walishindwa kutofautisha kati ya waanzilishi wa Jumuia ya zamani ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977 na waanzilishi wa jumuia mpya ya Afrika Mashariki ambayo mkataba wake ulisainiwa Arusha –

Tanzania mwaka 1999 na jumuia ikaanza kufanya kazi mwaka 2000. Watahiniwa hawa walitakiwa kuelewa kuwa Julius Nyerere, Jomo Kenyata na Milton Obote walianzisha Jumuia ya zamani ya Afrika mashariki mwaka 1967.

Kipotoshi B, Julius Nyerere, Daniel Moi na Yoweri Museveni kiliwavutia watahiniwa 126,861 (13.59%) ambao hawakuwa na uelewa wa waanzilishi wa Jumuia mpya ya Afrika Mashariki. Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kuwa Julius Nyerere hakuwa mmoja wa waanzilishi wa Jumuia mpya ya Afrika Mashariki kwani aliachia madaraka mwaka 1985 karibia miaka 14 kabla ya kuanzishwa kwa Jumuia mpya ya Afrika Mashariki mwaka 1999.

Vipotoshi C, *Jakaya Kikwete, Daniel Moi na Yoweri Museveni* (6.67%) na D, *Benjamin Mkapa, Uhuru Kenyatta na Yoweri Museveni* (12.27%) vilichaguliwa na watahiniwa ambao hawakuelewa kuwa Jakaya Kikwete aliingia madarakani mwaka 2005 – miaka sita baada ya kuanzishwa tena kwa Jumuia mpya ya Afrika Mashariki ilhali Uhuru Kenyatta aliingia madarakani mwaka 2013 miaka 15 baada ya kuanzishwa upya kwa Jumuia mpya ya Afrika Mashariki.

Pamoja na hayo, ni watahiniwa 135,682 (14.54%) tu waliweza kuchagua jibu sahihi E, Yoweri Museveni, Daniel Moi na Benjamin Mkapa. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ushirikiano wa kimataifa. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kimeoneshwa katika Chati Na. 14



**Chati Na. 14** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 26.*

### 2.1.3. Kipengele III: Jiografia

**Swali la 27:** Tabia nchi ambayo ina sifa ya joto kali na mvua nyingi katika kipindi chote cha mwaka hujulikana kama

A Ikweta B Jangwa

C Tropiki D Nusujangwa

E Milimani.

**Jedwali 10: Idadi na wastani wa watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 418,125 | 149,630 | 206,448 | 92,625 | 60,265 | 6,250 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 44.80 | 16.03 | 22.12 | 9.92 | 6.46 | 0.67 |

Katika jedwali la 10 Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni cha wastani kwani asilimia 44.80 walichagua jibu sahihi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mazingira.* Swali liliwataka watahiniwa kubainisha tabia nchi ambayo ina joto kali na mvua nyingi katika kipindi chote cha mwaka. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani jumla ya watahiniwa 418,125 (44.80%) walichagua jibu sahihi *A, Ikweta*. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu tabia nchi yenye sifa ya kuwa na joto kali na mvua nyingi katika kipindi chote cha mwaka, hivyo kuchagua jibu sahihi.


Jumla ya watahiniwa 206,448 (22.12%) walichagua kipotoshi *C, Tropiki.* Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha sifa ya tabia nchi ya Tropiki na ya Ikweta. Katika eneo la Tropiki hali ya joto hujitokeza katika miezi ya Juni na Septemba, Novemba na April. Katika miezi mingine kuna baridi kali na mvua hunyesha kuanzia mwezi Oktoba hadi Machi.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 126,*861* (16.03%) walichagua kipotoshi *B, Jangwa,* na watahiniwa 92,625 (9.92%) walichagua kipotoshi *D*, *Nusujangwa*. Tabia nchi ya jangwa ina sifa ya

kuwa na mvua chache sana katika kipindi chote cha mwaka, wakati tabia nchi ya nusujangwa huwa na kiasi kidogo cha mvua na joto kali wakati wa mchana. Hivyo, watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu sifa za tabia nchi ya Ikweta ambayo ni joto kali na mvua nyingi katika kipindi chote cha mwaka hivyo walichagua majibu haya kwa kubahatisha.

Aidha, watahiniwa 60,265 (6.46%) waliochagua kipotoshi *E, Milimani* walishindwa kutofautisha Ikweta na milima. Milima ina tabia ya kuwa na mvua nyingi katika upande wa mlima unaopokea upepo (joshi). Upande huo wa mlima unazuia unyevu unaopita katika eneo hilo, hivyo kuwezesha kupata mvua ya kutosha katika kipindi kirefu cha mwaka, wakati upande usiopokea upepo (upande wa demani) unakuwa mkavu.

Chunguza kwa makini picha ifuatayo na kisha jibu swali la 28 na 29.




**Swali la 28;** Picha inaonesha nini?

A Hali ya hewa yenye ukosefu wa mvua
B Hali ya hewa yenye mvua nyingi
C Hali ya hewa yenye unyevunyevu mwingi
D Hali ya hewa yenye upepo mkali
E Hali ya hewa yenye kuganda kwa barafu

Swali hili lilitoka katika mada ya *Tafsiri ya Picha na Ramani*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kutafsiri picha na kisha kubainisha hali ya hewa inayoonekana katika picha. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri kwa sababu jumla ya watahiniwa

802,950 sawa na asilimia 86.03 waliweza kuchagua jibu sahihi A *Hali ya hewa yenye ukosefu wa mvua*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu namna ya kutafsri picha. Hivyo, waliweza kubaini hali ya hewa iliyooneshwa katika picha hiyo kwa kuhusianisha na vitu vinavyooneka katika picha. Picha inaonesha jinsi mazingira na uoto wa asili ulivyoathiriwa na shughuli za binadamu. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kimeoneshwa katika Chati Na. 15.




**Chati Na. 15** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 28.*

Watahiniwa walioshindwa kuchagua jibu sahihi hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada ya tafsiri ya picha na ramani na kuhusisha na mada ya hali ya hewa. Watahiniwa hao walishindwa kubaini uhusiano uliopo baina ya vitu vilivyowasilishwa katika picha na hali ya hewa. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *B, Hali ya hewa yenye mvua nyingi* (5.59%) *na C, Hali ya hewa yenye unyevunyevu mwingi* (2.15); walishindwa kubaini kuwa eneo lenye mvua nyingi na hali ya hewa yenye unyevu husababisha wanyama na mimea kustawi vizuri, wakati hali ya hewa yenye ukosefu wa mvua husababisha wanyama na mimea kufa.

Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *D, Hali ya hewa yenye upepo mkali ,(*3.74%) walishindwa kubaini kuwa upepo mkali huweza kung'oa miti pindi unapotokea*.* Hata hivyo, picha iliyotumika haikuwa na kiashiria chochote cha upepo mkali kama vile miti iliyong'oka au kuinamia upande mmoja. Pia, watahiniwa waliochagua *E, Hali ya hewa*

*yenye kuganda kwa barafu,(*2.18%) walishindwa kubaini kuwa mimea na wanyama husitawi vizuri katika eneo lenye barafu. Watahiniwa 2,912 ambao ni sawa na asilimia 0.31 hawakujibu kabisa swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 29**: Eneo linaloonekana katika picha limepatwa na janga gani?

| | | |
|---|---|---|
| A Mafuriko | B Ukame | C Vita |
| D Kimbunga | E Mlipuko wa volkano | |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Tafsiri ya Picha na Ramani*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa katika kutafsiri dhana iliyowasilishwa katika picha na kubainisha janga lililoathiri eneo husika. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri, ambapo jumla ya watahiniwa 802,717 sawa na asilimia 86.00 walichagua jibu sahihi *B, Ukame.* Ukame hutokea katika eneo ambalo mazingira ya asili yameharibiwa na shughuli mbalimbali za binadamu kama vile kilimo cha kuhama, uchimbaji wa madini, ukataji wa miti kwa ajili ya mbao, nguzo za kujengea nyumba na kuchoma mkaa wa kupikia. Shughuli hizo huathiri viumbe hai kama wanyama na mimea. Picha inaonesha hali ya ukame ulivyoathiri mimea na wanyama katika hilo eneo.

Watahiniwa waliochagua kipotoshi *A, Mafuriko* (5.34%) walishindwa kubaini kuwa mafuriko hayasababishwi na ukosefu wa mvua bali husababishwa na mvua nyingi zinazonyesha kwa muda mrefu. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *C, Vita (*2.44%) walishindwa kubaini athari ya kimazingira inayoonekana katika picha kuwa imesababishwa na ukame na siyo vita. Kukauka kwa miti, maji, kufa na kudhoofika kwa wanyama husababishwa kwa kiasi kikubwa na hali ya hewa yenye ukame.

Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotishi *D, Kimbunga, (*3.35%) walishindwa kubainisha kuwa mara nyingi kimbunga husababisha kung'olewa kwa miti na si kukauka kwa mimea na wanyama kama inavyoonekana katika picha. Aidha, watahiniwa waliochagua *E, Mlipuko wa volkano (*2.52%) tukio ambalo mara nyingi husababisha kufunikwa kwa ardhi kutokana na lava inayosambaa. Pia, husababisha kulipuka kwa moto nyikani na mjini. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada inayohusu picha hivyo walichagua majibu ambayo hayakuendana na matakwa ya swali.

**Swali la 30:** Nini faida ya utabiri wa hali ya hewa?

A Kuchukua tahadhari ya majanga
B Kuzuia majanga
C Kulinda mazingira
D Kujenga nyumba imara
E Kuepuka mafuriko

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Hali ya Hewa.* Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini faida ya utabiri wa hali ya hewa. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri kwani jumla ya watahiniwa 639,223 sawa na asilimia 68.49 walichagua jibu sahihi *A, Kuchukua tahadhari za majanga*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu faida ya utabiri wa hali ya hewa na jinsi unavyoweza kusaidia kuchukua tahadhari mapema ili kuyakabili majanga kabla hayajaleta madhara kwa binadamu na miundombinu.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa 300,486 sawa na asilimia 31.51, walichagua vipotoshi *B, Kuzuia majanga*, (8.05%); *C, Kulinda mazingira*, (12.69%); *D, Kujenga nyumba imara,* (4.76%) *E, Kuepuka mafuriko*, (5.33%). Uchaguzi wa vipotoshi hivi unadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu faida ya utabiri wa hali ya hewa na jinsi unavyoweza kusaidia katika kuchukua tahadhari pale mabadiliko ya hali ya hewa yanapotokea.

Watahiniwa waliochagua kipotoshi *B, Kuzuia majanga,* (8.05%); walishindwa kuelewa kuwa ni vigumu kuzuia janga kutokea bali taarifa za utabiri zinaweza kutumika kupunguza madhara ya janga hilo kwa watu kuchukua tahadhari. Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi *C, Kulinda mazingira,* (12.69%) walishindwa kubaini kuwa hakuna uhusiano uliopo baina ya kulinda mazingira na faida ya utabiri wa hali ya hewa.

Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi *D, Kujenga nyumba imara,* (4.76%) walishindwa kuelewa kuwa baadhi ya majanga yanakuwa na madhara makubwa kiasi ambacho nyumba imara haziwezi kuyazuia kutokana na ukubwa, nguvu au kasi yake. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *E, Kuepuka mafuriko,* (5.33%) walishindwa kubaini kuwa utabiri wa hali ya hewa hauondoi uwezekano wa kutokea mafuriko bali

huwezesha watu kuchukua tahadhari kama vile kuondoka maeneo hatarishi.

**Swali la 31:** Kwa nini watu walioko Mashariki huona jua mapema kuliko wale walioko Magharibi?

A Jua liko upande wa Mashariki mwa Dunia


B Dunia hujizungusha katika mhimili wake kutoka Magharibi kwenda Mashariki

C Dunia hujizungusha katika mhimili wake kutoka Mashariki kwenda Magharibi

D Kwa sababu mhimili wa dunia umekaa tenge

E Jua lipo upande wa Magharibi mwa Dunia

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Mfumo wa Jua.* Swali lilipima uwezo wa watahiniwa katika kubaini sababu ya watu walioko mashariki kuliona jua mapema kuliko wale walioko magharibi. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani ni watahiniwa 269,918 (28.92%) tu waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Dunia hujizungusha katika mhimili wake kutoka magharibi kwenda mashariki.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mfumo wa jua na matokeo ya mzunguko wa sayari ya Dunia katika mhimili wake kutoka Magharibi kwenda Mashariki. Mzunguko huu hukamilika kwa masaa 24 kutokana na dunia kujizungusha kutoka magharibi kwenda mashariki hivyo kufanya jua lionekane linachomoza mashariki na kuzama magharibi hivyo kuwafanya watu walioko Mashariki kuliona jua mapema kuliko wale walioko magharibi. Kufaulu kwa watahiniwa kumeoneshwa katika Chati Na. 16.





**Chati Na. 16** *Asilimia ya ufaulu wa watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 31.*

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 668,009 (70.33%) walichagua majibu yasiyo sahihi *A,* C, D na E*.* Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sayari ya Dunia kujizungusha katika mhimili wake na matokeo yake. Hivyo, walishindwa kuelewa sababu inayowawezesha watu walioko mashariki kuliona jua mapema kuliko walio upande wa magharibi. Watahiniwa wengine 4,584 sawa na asilimia 0.75 hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 32:** Ipi ni hasara ya uvuvi wa asili?

A Kutumia zana rahisi
B Kupata ajira binafsi
C Kupata samaki bora
D Kuuza samaki kwa bei ya chini
E Kukamata samaki wadogo

Swali lilitoka katika mada ya *Shughuli za Kiuchumi*. Watahiniwa walitakiwa kubainisha hasara ya uvuvi wa asili. Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani jumla ya watahiniwa 603,705 sawa na asilimia 64.68 walichagua jibu sahihi *E, Kukamata samaki wadogo.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hasara zinazotokana na uvuvi wa asili. Uvuvi wa asili hutumia nyavu zenye matundu madogo yasiyokubalika kisheria kutumika katika kazi ya uvuvi. Zana za asili huweza kukamata samaki wadogo ambao hawajafika muda muafaka wa kuvunwa. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kumeoneshwa katika Chati Na. 17




**Chati Na. 17** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 32*

Chati Na. 17 inaonesha kiwango kizuri cha kufaulu kwa watahiniwa kwani asilimia 64.68 walichagua jibu sahihi.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 333,555 (35.32%) walichagua majibu yasiyo sahihi kwani hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hasara ya uvuvi wa kutumia zana za asili. Kwa mfano, watahiniwa waliochagua kipotoshi *A, Kutumia zana rahisi,* (8.24%) walivutiwa na jibu hili kwa sababu zana nyingi za asili upatikanaji wake sio wa gharama kubwa katika kutengeneza na kuzitumia. Aidha, watahiniwa waliochagua *D, Kuuza samaki kwa bei ya chini (16.10%)* walivutiwa nalo kwa sababu utamaduni umejengeka katika jamii kuwa vitu vya asili huuzwa kwa bei ndogo. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa swali liliwataka kubaini hasara ya uvuvi wa asili na sio namna ya kutumia zana za asili wala bei ya samaki wanaovuliwa kwa kutumia zana za asili.

Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi *B, Kupata ajira binafsi,* (5.52%) walishindwa kutambua kuwa hakikuwa na uhusiano na hasara ya uvuvi wa asili. Pia watahiniwa waliochagua *C; Kupata samaki bora, (4.59%)* walishindwa kubaini kuwa ni vigumu kupata samaki bora kwa sababu uvuvi wa asili hutumia zana zisizokubalika kisheria. Njia nyingi za uvuvi wa asili hutumia zana zisizokubalika kama makokolo na madema ambayo huweza kukamata samaki wadogo ambao hawajafika umri unaofaa kuvunwa. Watahiniwa wapatao 8,076 sawa na asilimia 0.87 walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 33:** Bainisha madhara ya ufugaji wa mifugo mingi katika eneo dogo.

A Mmomonyoko wa udongo
B Mazao bora ya mifugo
C Faida kubwa
D Utajiri
E Umaarufu

**Jedwali 11: Idadi na wastani wa watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 818,753 | 35,717 | 30,430 | 20,758 | 23,167 | 4,518 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 87.72 | 3.83 | 3.26 | 2.22 | 2.48 | 0.48 |

Katika jedwali la 11 kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni kizuri kwani asilimia 87.72 walichagua jibu sahihi.

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Shughuli za Kiuchumi.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha madhara ya ufugaji wa mifugo mingi katika eneo dogo. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri kwani watahiniwa 818,753 sawa na asilimia 87.72 walichagua jibu sahihi *A, Mmomonyoko wa udongo.* Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu madhara yatokanayo na kufuga mifugo mingi katika eneo dogo kuwa huweza kusababisha mmomonyoko wa udongo. Mifugo inapopita eneo moja kwa muda mrefu husababisha udongo ulioshikamana kuachia na pia huharibu uoto juu ya udongo jambo ambalo husababisha tabaka la juu la udongo kuhathiriwa haraka na upepo au mvua. Eneo hilo likiathiriwa na mvua au upepo huondoa tabaka la juu la udongo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 110,073 ambao ni sawa na asilimia 11.79 hawakuzingatia matakwa ya swali kwani walichagua majibu yasiyo sahihi kama ifuatavyo*: B, Mazao bora ya mifugo (3.83*%)*; C, Faida kubwa (3.26*%); *D, Utajiri (2.22*%) *na E, Umaarufu (2.48*%).* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa vipotoshi hivi, vilikuwa vinaelezea sababu zinazofanya baadhi ya wafugaji kufuga mifugo mingi. Tabia hii ipo katika jamii za wafugaji ambapo kuwa na mifugo mingi ni sifa na humfanya mtu aonekane tajiri au maarufu.

**Swali la 34:** Lipi kati ya mambo yafuatayo **siyo** madhara yatokanayo na uharibifu wa misitu?

A Ongezeko la jangwa
B Ongezeko la ukame
C Upotevu wa madini
D Kupungua kwa mvua
E Kutoweka kwa viumbe hai

Swali lilitoka katika mada ya *Mazingira*. Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini jambo ambalo halitokani na uharibifu wa misitu. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 610,435 sawa na asilimia 65.40 walichagua jibu sahihi *C, upotevu wa madini.* Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu madhara yatokanayo na uharibifu wa misitu.

Kwa upande mwingine, asilimia 33.91 ya watahiniwa walichagua vipotoshi *A, ongezeko la jangwa (*8.04%); *B, ongezeko la , (*6.84%)*; D, kupungua kwa mvua (*8.23%) *na E, kutoweka kwa viumbe hai, (*10.80%) ambayo hayakuwa majibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha ufinyu wa maarifa waliokuwa nayo watahiniwa kuhusiana na madhara yatokanayo na uharibifu wa misitu. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa vipotoshi hivyo vyote ni madhara yatokanayo na uharibifu wa misitu.


**Swali la 35:** Vipi ni vyombo vya kisasa vya mawasiliano?

A Baragumu, runinga na simu ya mezani
B Redio, simu za mkononi na barua
C Barua, pembe na redio
D Ngoma, simu za mkononi na faksi
E Simu ya mezani, tarumbeta na redio

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha chaguo ambalo linahusisha vyombo vya kisasa vya mawasiliano. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 661,389 ambao ni sawa na asilimia 70.86 walichagua jibu sahihi *B, redio, simu za mkononi na barua.* Kufaulu huko kunaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vyombo vya mawasiliano hivyo kuweza kutofautisha vyombo vya kisasa vya mawasiliano na vyombo ambavyo siyo vya kisasa. Vyombo vya kisasa vya mawasiliano vilivyo vingi hutumia teknolojia ya kisasa, wakati vyombo vya kitamaduni/kizamani vya mawasiliano hutumia teknolojia duni.

Mfano wa vyombo vya kitamaduni/kizamani vya mawasiliano ni baragumu, moto, tarumbeta na ngoma.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 266,295 sawa na asilimia 28.53 hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, watahiniwa 117,052 ambao ni sawa na asilimia 12.54 walichagua *A, Baragumu, runinga na simu ya mezani*; 44,424 sawa na asilimia 4.76 walichagua *C, Barua, pembe na redio*; 36,655 sawa na asilimia 3.93 walichagua *D, Ngoma, simu za mkononi na faksi* na watahiniwa 68,164, sawa na asilimia 7.30 walichagua *E, Simu ya mezani, tarumbeta na redio*. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa machaguo hayo yote mojawapo ya vyombo vilikuwa ni vyombo vya kitamaduni/kizamani vya mawasiliano ambavyo ni *baragumu, pembe, ngoma* na *tarumbeta*. Asilimia 0.61 ya watahiniwa hawakujibu swali hili au walichagua majibu zaidi ya moja.




**Chati Na. 18** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 35*

**Swali la 36:** Zipi ni njia kuu za mawasiliano?

A Mdomo, maandishi na ishara
B Ngoma, simu za mezani na maandishi
C Barua, moto na ngoma
D Simu za mkononi, simu za mezani na ngoma
E Barua, televisheni na redio

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi*. Swali liliwataka watahiniwa kubainisha njia kuu za mawasiliano katika

machaguo waliyopewa. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 428,640 ambao ni sawa na asilimia 45.93 walichagua jibu sahihi *A*, *Mdomo, maandishi na ishara.* Watahiniwa hao walielewa kuwa watu huwasiliana kwa kutumia njia za mdomo kwa kutamka maneno mbalimbali, maandishi kama vile barua au kwa ishara ambayo hutumika hasa kwa viziwi na bubu ambao hawasikii na hawawezi kutamka maneno.

Watahiniwa wengi (53.17%) hawakuelewa vizuri mada ndogo juu ya *njia kuu za mawasiliano*. Kwa mfano, watahiniwa 48,618 ambao ni sawa na asilimia 5.21 walichagua *B, Ngoma, simu za mezani na maandishi*; 33,818 (3.62%) walichagua kipotoshi *C, Barua, moto na ngoma*; 105,416 sawa na asilimia 11.29 walichagua kipotoshi *D, Simu za mkononi, simu za mezani na ngoma*; na watahiniwa, 308,503 sawa na asilimia 33.05 walichagua kipotoshi *E, Barua, televisheni na redio*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi B, C, D na E walishindwa kutambua kuwa machaguo haya yote yalihusisha vyombo vinavyotumika katika mawasiliano na siyo njia za mawasiliano. Watahiniwa wengine asilimia 0.89 waliobaki hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 37:** Mimi ni gimba la tatu kutoka jua lilipo. Jua ni rafiki yangu. Nakaa umbali wa kilometa milioni 149 kutoka kwenye jua. Ninalizunguka jua kwa siku 365 $\frac{1}{4}$. Ukubwa wangu ni mara tatu ya lile gimba la kwanza. Mimi ni nani?

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A | Mirihi | B | Dunia | C | Zohari |
| D | Kausi | E | Sumbula | | |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mfumo wa Jua.* Katika kujibu swali hili, watahiniwa walitakiwa kubaini sayari ambayo ina sifa zilizotajwa katika swali. Kiwangi cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 697,389 ambao ni sawa na asilimia 74.72 walichagua jibu sahihi *B*, *Dunia.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sifa mbalimbali za sayari Dunia kama vile ni gimba la tatu kutoka jua lilipo, iko umbali wa kilometa milioni 149 kutoka kwenye jua, ukubwa wake ni mara tatu ya lile gimba la kwanza na hulizunguka jua kwa siku 365 $\frac{1}{4}$.

Watahiniwa wengine 242,057 sawa na asilimia 24.63 hawakuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa hawa walivutiwa na vipotoshi *A, Mirihi* (4.78%); *C, Zohari* (6.90%); *D, Kausi* (5.36%); na *E, Sumbula* (7.59%).

Watahiniwa hao hawakuzingatia sifa mbalimbali za sayari zilizotajwa katika swali. Hali hii inaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa sifa mbalimbali za sayari katika mfumo wa jua.

**Swali la 38:** Chanzo cha maji kinachopatikana kwa kuchimba shimo refu chini ya ardhi huitwa

A mto. B ziwa. C bwawa.
D kisima. E bahari.

**Jedwali 12: Idadi na wastani wa watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 32,231 | 45,364 | 62,256 | 753,623 | 34,422 | 5,447 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 3.45 | 4.86 | 6.67 | 80.74 | 3.69 | 0.58 |

Katika jedwali la 12 kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ni kizuri kwani asilimia 80.74 walichagua jibu sahihi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maji.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha jina la chanzo cha maji kinachopatikana kwa kuchimba shimo refu chini ya ardhi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri kwani watahiniwa 753,623 ambao ni sawa na asilimia 80.74 waliweza kuchagua jibu sahihi *D, kisima*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sifa za vyanzo mbalimbali vya maji.

Aidha, chaguo *A, mto* liliwavuta watahiniwa 32,231 ambao ni sawa na asilimia 3.45. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa mto ni chanzo cha maji kinachotiririka juu ya ardhi. Pia, watahiniwa 45,364 sawa na asilimia 4.86 walichagua kipotoshi *B, ziwa*; watahiniwa 62,256 sawa na asilimia 6.67 waliochagua *C, bwawa* na watahiniwa 34,422 ambao ni sawa na asilimia 3.69 walichagua *E, Bahari*. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A, B, C na E walishindwa kubaini kuwa vyanzo hivyo vya maji viko juu ya usawa wa ardhi na havipatikani kwa kuchimba shimo refu chini ya ardhi.


**Swali la 39:** Viwanda vinachangiaje uchafuzi wa vyanzo vya maji?

A Kwa kujenga mabwawa.
B Kwa kuelekeza mifumo ya maji taka mtoni.
C Kwa kufanya matumizi mrudio ya takataka.
D Kwa kujenga mifumo ya maji taka.
E Kwa kutumia nishati ya nguvu za maji.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maji.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha njia za uchafuzi wa vyanzo vya maji, hasa uchafuzi unaofanywa na viwanda. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 576,291 ambao ni sawa na asilimia 61.74 walichagua jibu sahihi *B, kwa kuelekeza mifumo ya maji taka mtoni*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa njia kuu inayotumiwa na viwanda kuchafua vyanzo vya maji ni kwa kuelekeza mifumo ya maji taka mtoni. Maji taka hayo yanakuwa na kemikali mbalimbali na uchafu hivyo yanapofika mtoni huchafua maji.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua kipotoshi *A, kwa kujenga mabwawa,* (4.64%) na *D, kwa kujenga mifumo ya maji taka,* (8.08%) walishindwa kubaini kuwa hizi ni njia salama za kuhifadhi maji taka ambazo hazisababishi uchafuzi wa vyanzo vya maji. Aidha, watahiniwa 100,589 ambao ni sawa na asilimia 10.78% waliochagua kipotoshi E*, kwa kutumia nishati ya nguvu za maji;* walishindwa kubaini kuwa haya ni matumizi salama ya maji kwa sababu maji yanapotumika kuzalisha nishati ya umeme hayasababishi uchafuzi wa vyanzo vya maji.

Vilevile, watahiniwa 131,670 sawa na asilimia 14.11 waliochagua kipotoshi *C, kwa kufanya matumizi mrudio ya takataka* hawakuelewa kuwa kwa kufanya matumizi mrudio ya takataka, kunasababisha kutokuwepo kwa takataka ambazo zitaelekezwa katika vyanzo vya maji na kusababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji. Hata hivyo, asilimia 0.65 ya watahiniwa hawakujibu swali hili, au walichagua jibu zaidi ya moja. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kimeoneshwa katika Chati Na. 19.





**Chati Na. 19** *Asilimia ya watahiniwa katika kila chaguo katika swali la 39.*

**Swali la 40:** Lipi ni jina la sayari ya pili kwa ukubwa katika mfumo wa Jua?

A Zebaki B Mirihi C Sarateni
D Dunia E Sumbula

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mfumo wa Jua.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha jina la sayari ya pili kwa ukubwa katika mfumo wa Jua. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango hafifu kwani watahiniwa 264,919 ambao ni sawa na asilimia 28.38 waliweza kuchagua jibu sahihi *C, Sarateni*. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sifa mbalimbali za sayari katika mfumo wa jua.

Watahiniwa wengine waliochagua kipotoshi *A, Zebaki*, 214,739 (23.01%) walishindwa kubaini kuwa sayari hii ni ndogo kuliko sayari zote katika mfumo wa jua. Kipotoshi *B, Mirihi*, kilivutia watahiniwa 110,090 (11.80%), ambao walishindwa kubaini kuwa hii ni sayari ya saba kwa ukubwa katika mfumo wa jua. Kipotoshi *D, Dunia* kiliwavutia watahiniwa 146,669 (15.71%) ambao walishindwa kubaini kuwa hiyo ni sayari ya tano kwa ukubwa katika mfumo wa jua. Watahiniwa 189,497 (20.30%) waliochagua kipotoshi *E, Sumbula*,walishindwa kubaini kuwa hiyo ni sayari ya kwanza kwa ukubwa katika mfumo wa jua. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kimeoneshwa katika Chati Na. 21.





**Chati Na. 20** *kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 40*

## 2.2. Sehemu B

**Swali la 41:** Kwa nini Katiba ya nchi inajulikana pia kama sheria mama ya nchi?

Swali lilitoka katika mada ya *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu dhana ya Katiba ya nchi. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa kilikuwa hafifu ambapo watahiniwa 121,774 (13.05%) waliokuwa na maarifa ya kutosha walipata alama kuanzia 1.5 hadi 2. Watahiniwa wengine 103,893 (11.13%) walipata alama 1 na watahiniwa 707,682 (75.82%) walipata alama kuanzia 0 hadi 0.5. Chati Na. 21 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 41.




**Chati Na. 21** *Asilimia ya watahiniwa na alama walizopata.*

Watahiniwa waliopata alama kuanzia 0 hadi 0.5 (75.82%) walitoa hoja mbalimbali kinyume na matakwa ya swali zikiwemo: *katiba ya nchi ni sheria mama ya nchi kwa sababu hakuna aliye juu ya sheria*; *katiba ya nchi ni sheria mama ya nchi kwa sababu inahusu haki za kina mama; kwa sababu katiba inatiwa sahihi na Rais; kwa sababu ni katiba iliyoundwa na vyama viwili vya siasa ASP na TANU;* na *katiba inatumika mahakamani.* Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya katiba ya nchi. Kielelezo Na. 1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyoendana na matakwa ya swali.

| |
|---|
| 41. Kwa nini Katiba ya nchi inajulikana pia kama sheria mama ya nchi?<br>Kwasababu unausu haki za Kina mama |

**Kielelezo Na. 1:** *Kinaonesha jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali la 41.*


Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (13.05%) walipata alama kuanzia 1.5 hadi 2, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya katiba ya nchi na kueleza kwa nini katiba ya nchi inajulikana pia kama sheria mama ya nchi. Katiba ni mwongozo wa msingi wa sheria zinazotungwa na kutumika nchini. Sheria yoyote inayotungwa kinyume na katiba ya nchi huwa batili. Kutokana na hilo, katiba ni sheria mama ya nchi. Baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa yalikuwa: *Sheria zingine zinatungwa kutokana na katiba ya nchi*; *Katiba hutumika kama mwongozo wa kutunga sheria zote katika nchi*. Vilevile, baadhi ya watahiniwa 103,893 (11.13%) walipata alama 1 kutokana na kutoa hoja ambazo hazikujitosheleza kupata alama zote 2 stahiki katika swali hili. Kielelezo Na. 2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwenye maarifa ya kutosha.

| |
|---|
| 41. Kwa nini Katiba ya nchi inajulikana pia kama sheria mama ya nchi?<br>Kwasababu sheria zingine zinatungwa kuto kana na katiba |

**Kielelezo Na. 2:** *Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa aliyejibu swali hili*.

**Swali la 42:** Eleza manufaa mawili yaliyopatikana kutokana na kukomeshwa kwa biashara ya utumwa katika Tanganyika.

Swali liliwataka watahiniwa kueleza manufaa mawili yaliyopatikana kutokana na kukomeshwa kwa biashara ya utumwa katika Tanganyika. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa ni dhaifu kwani ni watahiniwa 199,225 (21.35%) tu waliweza kueleza manufaa yaliyopatikana kutokana na kukomeshwa biashara ya utumwa katika Tanganyika. Aidha, jumla ya watahiniwa 282,958 sawa na asilimia 30.31 walipata alama kati ya 0.5 na 1.5. Watahiniwa wengi (451,166 sawa na asilimia 48.34) walipata alama sifuri kwa sababu walikosa maarifa kwenye mada iliyotahiniwa. Watahiniwa katika sampuli hii baadhi yao walitaja jamii za watu/mataifa zilizoshiriki/yaliyoshiriki katika biashara ya utumwa au njia zilizotumika kuwapata watumwa. Baadhi ya majibu yasiyo sahihi yaliyotolewa na watahiniwa ni kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na.3.


42. Eleza manufaa mawili yaliyopatikana kutokana na kukomeshwa kwa biashara ya utumwa katika Tanganyika.


(a) Wareno

(b) wanyimwemi

***Kielelezo Na 3** sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilo sahihi*.

**Swali la 43:** Vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi za Kiafrika husababishwa na nini?Eleza sababu mbili.

Swali hili liliwataka watahiniwa kueleza sababu mbili zinazosababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi za Kiafrika. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa ni dhaifu kwani watahiniwa wengi (493,897 sawa na asilimia 52.92) walipata alama sifuri. Watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na uelewa kuhusu mada iliyotahiniwa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.4.


43. Vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi za Kiafrika husababishwa na nini? Eleza sababu mbili.

(a) uChafuzi wamazingira


(b) Sungusungu

*__Kielelezo Na.4__ sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza sababu zinazosababisha machafuko katika nchi za kiafrika.*

Aidha, watahiniwa 327,028 sawa na asilimia 35.03 walipata alama kati ya 0.5 na 1.5 na watahiniwa 112,424 (12.05%) tu walipata alama 2. Watahiniwa waliopata alama 2 walieleza jinsi athari za ukoloni, ukabila, rushwa na kugombania madaraka kunavyochangia kuzuka kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe katika Afrika.

Soma Kwa makini ramani ifuatayo kisha jibu swali la 44

**RAMANI YA TANZANIA**




**Swali la 44**: Mto uliopewa herufi **C** hutenganisha nchi zipi?


(a) ____________________

____________________

(b) ______________________________________________

______________________________________________

Swali hili lilitoka katika mada ya *Usomaji wa Ramani.* Swali liliwataka watahiniwa kusoma ramani ya Tanzania kwa makini, kisha kutaja nchi mbili zinazotenganishwa na mto uliopewa herufi C. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwa sababu watahiniwa 429,068 sawa na asilimia 45.97 waliweza kuandika majibu sahihi *Tanzania na Msumbiji* hivyo kupata alama zote 02. Watahiniwa 247,688 sawa na asilimia 26.54 walipata alama 01 kwa kuandika jibu sahihi moja tu kati ya mawili. Aidha, watahiniwa 252,414 sawa na asilimia 27.04 walipata alama 0 kwa sababu waliandika majibu yote yasiyo sahihi.mtawanyiko huu wa kufaulu unaoneshwa katika chati ifuatayo:




**Chati Na. 22** *Takwimu za kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 44.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umebaini kuwa watahiniwa walioandika majibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nchi mbili zinazotenganishwa na mto uliopewa herufi C kuwa ni *Tanzania na Msumbiji.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu


ramani ya Tanzania,na kuweza kubaini kirahisi nchi inayopakana na Tanzania upande wa kusini.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 01 walishindwa kukidhi matakwa ya swali kwa kuchanganya majibu sahihi na yale yasiyo sahihi kama vile*: Tanzania na Zanzibar; Tanganyika na Msumbiji; Msumbiji na Malawi, na Malawi na Tanzania*. Majibu yote hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ramani ya Tanzania na hivyo kuandika majibu yasiyokuwa sahihi.

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa watahiniwa waliopata alama sifuri (0), hawakuwa na maarifa kuhusu *Stadi sahili za ramani,* kwani waliandika nchi kama; *Uingereza na Ujerumani; Misri na Malawi; Uganda na Kenya*. Pia, baadhi yao walionesha kuwa na mkanganyiko juu ya mahitaji ya swali kwani waliandika jina la mto uliopewa herufi C ni mto Ruvuma na Rufiji badala ya kubainisha nchi zinazotenganishwa na mto uliopewa herufi C.

**Swali la 45**: Eleza faida nne za mito.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Usomaji wa Ramani.* Swali lilipima uwezo wa mtahiniwa kueleza faida nne za mito. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani watahiniwa 422,624 sawa na asilimia 45.28 walieleza kwa usahihi faida nne za mito na kupata alama zote 02. Kwa upande mwingine, watahiniwa 143,960 sawa na asilimia 15.42 walifanikiwa kueleza kwa usahihi faida mbili za mito hivyo kupata alama 01. Hata hivyo, watahiniwa 89,611 ambao ni sawa na asilimia 9.60 walipata alama 0 kwani walishindwa kueleza faida nne za mito. Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 45 umeelezwa zaidi katika Chati Na. 23





**Chati Na. 23** *kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 45*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama 02 walieleza kwa usahihi faida nne za mito. Mfano wa majibu sahihi yaliyoandikwa na watahiniwa ni:

> *husaidia katika kilimo cha umwagiliaji, ni chanzo cha nishati ya umeme, hutumika katika uvuvi wa samaki, ni chanzo cha maji yanayotumika viwandani, inasaidia katika kutengeneza mvua, ni chanzo cha maji yanayotumika majumbani, ni chanzo cha chakula kama samaki, ni makazi kwa viumbe hai kama samaki* na *hutumika kama njia ya usafirishaji.*

Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu faida za mito. Kielelezo Na.5 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeweza kuandika majibu sahihi.



45. Eleza faida nne za mito.

(a) Kutengeza nishati ya umeme kupitia maji.

(b) Kumwagilia mashamba.

(c) Kufanganyia usafirishaji kwa kutumia vyombo mbalimbali kama Boti, mtumbwi na mashua.


(d) ~~Hutumi~~ maji yake Hutumika kwa kufulia, kuogea, kunywa n.k.

**Kielelezo 5** *Ni mfano wa majibu sahihi*

Hata hivyo, uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa walipata alama 01 kwani walieleza faida mbili zilizo sahihi kati ya nne. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *husaidia katika kilimo cha umwagiliaji, ni chanzo cha maji kwa ajili ya kuzalisha umeme, utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa vyanzo vya maji.* Majibu mawili ya mwanzo ni sahihi na mawili ya mwisho syo sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 0 walishindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo kushindwa kueleza faida nne za mito. Watahiniwa katika kundi hili walieleza majibu yote yasiyo sahihi tofauti na matakwa ya swali. Pia watahiniwa wengine waliandika majibu yasiyoendana kabisa na matakwa ya swali, mfano: *mikumi, mbuga, nyati na simba*. Wengine walipatwa na mkanganyiko kwa kuandika vyanzo vya maji kama; *mabwawa, mito, maziwa na bahari*. Majibu yanaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matakwa ya swali badala yake walikuwa wanajaza tu

nafasi zilizoachwa wazi. Kielelezo Na: 6 kinaonesha majibu yasiyo sahihi katika swali la 45.


45. Eleza faida nne za mito.

(a) feidanne zamito
Uhamiaji Tanzania
Tanzania

(b) Tanzania
mgambo la Tanzani
uhamiaji

(c) Kwaba wa bawa
mbama waba ba
mbayambayawa

(d) Kwakwabibuwa
Saha zamelonyesho
Basnala

**Kielelezo Na.6** *Mfano wa jibu la mtahiniwa lisilo sahihi*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

Uchambuzi wa mada zote 30 katika mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kufaulu kwa watahiniwa kwa viwango vinavyotofautiana. Kufaulu kwa watahiniwa kulikua kwa kiwango kizuri katika mada 9, kwa kiwango cha wastani katika mada 11 na hafifu katika mada 10. Watahiniwa walibainishwa kuwa kufaulu kwa kiwango kizuri kulianzia asilimia 60 -100, ambako kumeoneshwa kwa rangi ya kijani katika jedwali. Vilevile, watahiniwa walibainishwa kuwa wamefaulu kwa kiwango cha wastani kama wastani wa kufaulu kwao kulikuwa kati ya asilimia 40-59. Kufaulu kwa kiwango hiki kumeoneshwa katika Jedwali kwa rangi ya njano. Kwa upande mwingine, kufaulu kwa kiwango hafifu kama wastani wa kufaulu kulikua kati ya asilimia 0-39. Kufaulu kwa kiwango hiki kumeoneshwa katika jedwali kwa rangi nyekundu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, kufaulu kwa watahiniwa katika baadhi ya mada kumeongezeka mwaka huu 2019 ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2018. Ufaulu kwa watahiniwa katika mada moja

kumeongezeka kutoka katika ufaulu hafifu hadi kufikia ufaulu mzuri. Mada hiyo ni *Utamaduni Wetu* (51.07%), pia kuna ongezeko la kufaulu kutoka kiwango cha wastani hadi kufaulu kwa kiwango kizuri katika mada za *Misingi ya Demokrasia* (37.08%) na *Shughuli za Kiuchumi (30.35%)*. Vilevile, katika baadhi ya mada kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kimeongezeka kutoka kiwango hafifu hadi kiwango cha wastani. Mada hizo ni *Mazingira (15.71%), Mfumo wa jua (11.34%) na Usomaji wa ramani (31.02%)*. Kwa upande mwingine, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada za *Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa (14.39%), Uvamizi Wa Kikoloni Katika Africa Kuanzia Mwaka 1880 (23.33%) na Mawasiliano, Biashara Na Uchukuzi* (7%) kimeshuka kutoka kiwango kizuri hadi kiwango cha wastani. Mada za *utamaduni wa Tanzania na tamaduni zingine (31.42%0, Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu (10.61%), Ushirikiano wa Kimataifa (2.29%) na Vitangulizi vya ukoloni (25.32%)* kulishuka kutoka kufaulu kwa kiwango cha wastani hadi kufaulu kwa kiwango hafifu.

Kwa ujumla, ulinganifu wa kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2019 umeonesha kuongezeka ukilinganisha na ule wa 2018. Hata hivyo, kwa kuangalia idadi ya mada zilizoongezeka kiwango cha kufaulu inalingana na idadi ya mada zilizoshuka kiwango cha kufaulu. Muhtasari wa viwango vya kufaulu katika kila mada zilizotahiniwa mwaka 2019 zimeoneshwa katika majedwali.

**Jedwali Na. 13: Mada zilizoonesha ongezeko la kufaulu kwa watahiniwa**

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2018 (%) | Wastani wa ufaulu 2019 (%) | Wastani wa ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Utamaduni wetu | 28.42 | 79.49 | 51.07 |
| 2. | Misingi ya Demokrasia | 47.12 | 84.20 | 37.08 |
| 3. | Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa Mengine | 23.95 | 48.58 | 24.63 |
| 4. | Familia Yetu | 80.46 | 80.95 | 0.46 |

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2018 (%) | Wastani wa ufaulu 2019 (%) | Wastani wa ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| 5. | Mazingira | 39.39 | 55.1 | 15.71 |
| 6. | Mfumo wa Jua | 32.67 | 44.01 | 11.34 |
| 7. | Usomaji wa Ramani | 14.61 | 45.63 | 31.02 |
| 8. | Shughuli za Kiuchumi | 45.85 | 76.2 | 30.35 |

**Jedwali Na 14: Mada zilizoonesha kushuka kwa kufaulu kwa watahiniwa**

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2018 (%) | Wastani wa ufaulu 2019 (%) | Wastani wa kushuka (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ulinzi na usalama katika shule/Taifa | 66.34 | 51.95 | 14.39 |
| 2. | Uchumi wetu | 82.30 | 60.47 | 21.83 |
| 3. | Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni zingine | 49.46 | 18.04 | 31.42 |
| 4. | Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika Kuanzia Mwaka | 60.93 | 37.6 | 23.33 |

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2018 (%) | Wastani wa ufaulu 2019 (%) | Wastani wa kushuka (%) |
|---|---|---|---|---|
| | 1880 | | | |
| 5. | Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu | 59.61 | 14.5 | 10.61 |
| 6. | Ushirikiano wa Kimataifa | 56.61 | 14.5 | 2.29 |
| 7. | Vitangulizi vya Ukoloni | 48.78 | 30.15 | 25.32 |
| 8. | Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi | 65.39 | 58.39 | 7 |

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii umeonesha kuongezeka kwa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia 3.03 (hii ina maana kwamba, mwaka 2019 ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 73.62 mwaka 2018 hadi asilimia 76.63 mwaka 2019). Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mada 30 zilizotahiniwa mwaka 2019 kimeongezeka kutoka ufaulu hafifu hadi ufaulu mzuri katika mada moja ambayo ni; *Utamaduni Wetu*.

Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kimeongezeka kutoka kiwango cha wastani hadi kiwango kizuri katika mada mbili ambazo ni *Misingi* ya *Demokrasia* na *Shughuli za Kiuchumi*.

Vilevile, katika baadhi ya mada kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kimeongezeka kutoka kiwango hafifu hadi kiwango cha wastani. Mada hizo ni *Mazingira, Mfumo wa jua na Usomaji wa ramani*.

Aidha, kiwango cha kufaulu katika mada za *Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa, Uvamizi Wa Kikoloni Katika Africa Kuanzia Mwaka 1880 na Mawasiliano, Biashara Na Uchukuzi* kimeshuka kutoka kiwango kizuri hadi kiwango cha wastani. Mada za *utamaduni wa Tanzania na tamaduni zingine, Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu, Ushirikiano*

*wa Kimataifa na Vitangulizi vya ukoloni zi*meshuka kutoka kiwango cha wastani hadi kiwango hafifu.

Kwa ujumla, mada ya *Uongozi wa Serikali za Mitaa* imeendelea kuwa na kiwango hafifu cha kufaulu.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha elimu hususan kufaulu kwa watahiniwa. Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo;

(a) Ufundishaji na ujifunzanji wa mada zilizobainika kuwa na ufaulu hafifu ambazo ni *Uongozi wa Serikali za Mtaa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni Nyingine, Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu, Biashara ya Utumwa, Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni Katika Afrika, Vitangulizi vya kikoloni, Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika Kuanzia mwaka 1880, Ushirikiano wa Kimataifa na Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika huru* uzingatie mbinu mbalimbali za ufundishaji ikiwa ni pamoja na;

(i) Matumizi ya vikundi vya majadiliano na uwasilishaji wake ambao hujenga kumbukumbu ya kudumu kwa wanafunzi.

(ii) Kutegemea aina ya mada, walimu watumie njia ya kazi mradi katika kukazia maarifa wanayojifunza wanafunzi.

(iii) Kuwepo kwa mbinu ya matumizi ya igizo dhima ambalo huhusisha milango mingi ya fahamu hivyo kujenga kumbukumbu ya kudumu kwa wanafunzi.

(iv) Wanafunzi wawasilishe majibu kwa njia ya mdahalo wakati wa kujifunza mada mbalimbali ili kujenga ufahamu juu ya mada hizo.

(v) Kutumia mgeni/mtaalamu mwalikwa wa mada mbalimbali.

(vi) Kutegemea na aina ya mada kuwepo na michoro mbalimbali kufafanua dhana mbalimbali.

(vii) Kuwepo na matumizi ya maswali hojaji kwa ajili ya kutafiti taarifa za mada mbalimbali.

(b) Wanafunzi washauriwe na kusisitiziwa kusoma kwa bidii vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza maarifa na ujuzi ambao utawawezesha kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi.

(c) Walimu na wanafunzi wapitie taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi inayotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania ili kutambua makosa ya kimazoea yanayosababisha kushindwa kufanya vizuri mitihani ya mwisho na kuyarekebisha ipasavyo.

(d) Mamlaka husika ziendelee kufanya ufuatiliaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Uraia, Historia na Jiografia, hasa kutilia mkazo zaidi mada ambazo ufaulu wa watahiniwa umeshuka ili kubaini changamoto zinazozuia ufanisi katika ujifunzaji na ufundishaji na kuziondoa ili kuongeza kiwango cha kufaulu.

**KIAMBATISHO**

**Ulinganifu wa kufaulu kwa watahiniwa katika kila mada kwa mwaka 2018 na 2019**

| Na | Mada | Mtihani wa 2018 | | | | Mtihani wa 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni | Kufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | |
| 1. | Uongozi katika Ngazi ya Familia/Shule | 1 | 68.39 | 68.39 | Vizuri | - | - | - | - |
| 2. | Uongozi wa Serikali za Mitaa | 2 | 20.23 | 36.08 | Hafifu | 2 | 11.48 | 11.48 | Hafifu |
| | | 3 | 51.92 | | | | | | |
| 3. | Serikali Kuu | - | - | - | - | 12 | 58.31 | 58.31 | Wastani |
| 4. | Demokrasia | - | - | - | - | 5 | 51.95 | 51.95 | Wastani |
| 5. | Alama za shule/ Taifa | 4 | 72.19 | 72.19 | Vizuri | 1 | 74.75 | 74.75 | Vizuri |
| 6. | Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa | 11 | 66.34 | 66.34 | Vizuri | 6 | 38.32 | 51.95 | Wastani |
| | | | | | | 11 | 68.58 | | |
| 7. | Uchumi Wetu | 5 | 82.30 | 82.30 | Vizuri | 10 | 60.47 | 60.47 | Vizuri |
| 8. | Utamaduni Wetu | 7 | 28.42 | 28.42 | Hafifu | 9 | 79.49 | 79,49 | Vizuri |
| 9. | Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa Mengine | 9 | 23.95 | 23.95 | Hafifu | 7 | 48.58 | 48.58 | Wastani |
| 10. | Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | - | - | - | - | 4 | 14.18 | 34.77 | Hafifu |
| | | | | | | 41 | 69.53 | | |
| 11. | Misingi ya Demokrasia | 6 | 61.84 | 47.12 | Wastani | 3 | 84.20 | 84.20 | Vizuri |
| | | 8 | 25.53 | | | | | | |
| | | 10 | 81.72 | | | | | | |
| | | 41 | 19.37 | | | | | | |
| 12. | Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni | 12 | 49.46 | 49.46 | Wastani | 8 | 18.04 | 18.04 | Hafifu |

| Na | Mada | Mtihani wa 2018 | | | | Mtihani wa 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni | Kufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | |
| | Nyingine | | | | | | | | |
| 13. | Familia Yetu | 13 | 87.90 | 80.46 | Vizuri | 14 | 80.71 | 80.95 | Vizuri |
| | | 22 | 80.57 | | | 15 | 81.22 | | |
| | | 23 | 72.91 | | | | | | |
| 14. | Shule Yetu | - | - | - | - | 16 | 61.58 | 61.58 | Vizuri |
| 15. | Kijiji Chetu | - | - | - | - | 18 | 40.84 | 40.84 | Wastani |
| 16. | Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu | 19 | 59.61 | 59.61 | Wastani | 23 | 48.99 | 48.99 | Wastani |
| 17. | Hatua za Maendeleo ya Binadamu Katika Zama Mbalimbali | 20 | 53.90 | 53.90 | Wastani | - | - | - | - |
| 18. | Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala Katika Jamii za Kitanzania hadi Karne ya 19. | 21 | 19.59 | 19.59 | Hafifu | - | - | - | - |
| 19. | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu | - | - | - | - | 22 | 32.76 | 32.76 | Hafifu |
| 20. | Biashara ya Utumwa | - | - | - | - | 42 | 21.35 | 21.35 | Hafifu |
| 21. | Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Tanganyika na Zanzibar | 24 | 44.35 | 44.35 | Wastani | - | - | - | - |
| 22. | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar | 14 | 56.70 | 45.60 | Wastani | - | - | - | - |
| | | 18 | 41.80 | | | | | | |
| | | 42 | 38.36 | | | | | | |
| 23. | Kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni katika Afrika | - | - | - | - | 17 | 4.98 | 17.17 | Hafifu |
| | | | | | | 20 | 17.12 | | |
| | | | | | | 21 | 29.38 | | |

| Na | Mada | Mtihani wa 2018 | | | | Mtihani wa 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | | | Kufaulu kwa kila Swali | | | |
| | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| 24. | Vitangulizi vya kikoloni | 17 | 48.78 | 48.78 | Wastani | 13<br>24 | 26.93<br>33.37 | 30.15 | Hafifu |
| 25. | Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika kuanzia mwaka 1880 | 15 | 65.37 | 60.93 | Vizuri | 19 | 37.56 | 37.56 | Hafifu |
| 26. | Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru | - | - | - | - | 25-<br>43 | 23.55<br>12.05 | 18.05 | Hafifu |
| 27. | Ushirikiano wa Kimataifa | 25 | 52.00 | 56.61 | Wastani | 26 | 14.54 | 14.54 | Hafifu |
| 28. | Mawasiliano, biashara na uchukuzi | 38<br>39<br>38 | 64.52<br>72.23<br>64.52 | 65.39 | Vizuri | 35<br>36 | 70.86<br>45.93 | 58.39 | Wastani |
| 29. | Mazingira | 31<br>33<br>34 | 74.34<br>23.26<br>20.58 | 39.39 | Hafifu | 27<br>34 | 44.80<br>65.40 | 55.1 | Wastani |
| 30. | Shughuli za Kiuchumi | 37 | 45.85 | 45.85 | Wastani | 32<br>33 | 64.68<br>87.72 | 76.2 | Vizuri |
| 31. | Usomaji wa ramani | 32<br>45 | 23.22<br>6.01 | 14.61 | Hafifu | 44<br>45 | 45.97<br>45.28 | 45.63 | Wastani |
| 32. | Maji | 29 | 60.84 | 60.84 | Vizuri | 38<br>39 | 80.74<br>61.74 | 71.24 | Vizuri |
| 33. | Mfumo wa Jua | 44 | 32.67 | 32.67 | Hafifu | 31<br>37<br>40 | 28.92<br>74.72<br>28.38 | 44.01 | Wastani |
| 34. | Hali ya hewa | 35 | 74.19 | 74.19 | Vizuri | 30 | 68.49 | 68.49 | Vizuri |
| 35. | Tafsiri ya Picha na ramani | | | | | 28<br>29 | 86.03<br>86.00 | 86.02 | Vizuri |
| 36. | Kutegemeana katika mazingira | 30 | 71.30 | 71.30 | Vizuri | - | - | - | - |
| 37. | Majanga | 27<br>28 | 53.81<br>67.29 | 60.55 | Vizuri | - | - | - | - |
| 38. | Idadi ya Watu na Makazi | 36 | 59.67 | 59.67 | Wastani | - | - | - | - |